epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumamosi Julai 13, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581736
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



## FA KUMBAKIZA SOUTHGATE KOCHA ENGLAND

UKURASA 21

UKURASA WA 2

**Uhakiki** w'biashara soko jipya Kariakoo sasa kufanyika upya



UKURASA WA 3

**Kuenguliwa** kina Wakili Mwabukusi kwazidi kuchafua hali ya hewa TLS

UKURASA WA 17

**Kenya** bado kuna fukuto, IGP ajiuzulu

# Wateja 'wanavyopigwa' ununuzi nyama buchani

UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimia wananchi baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Mpanda, Mkoa wa Katavi kwa ajili ya kuanza ziara ya kikazi mkoani humo jana. **PICHA: IKULU**

## Dk. Tulia, Rais Putin wateta vita vya Russia, Ukraine

UKURASA 2



UDANGANYIFU VYUONI

# Wazazi waangua kilio ofisini kwa Waziri Mkenda

• **Mbinu** kunasa tasnifu za wizi PhD, shahada ya uzamili... *Endelea Uk. 5*

**MICHEZO** **SIMBA YATAMBA KUONESHA UKUBWA CAF** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Uhakiki wafanyabiashara soko jipya Kariakoo kufanyika upya

**Na Halfani Chusi**

SIKU moja baada ya wafanyabiashara wa Soko Kuu la Kimataifa Kariakoo kuandamana kwenda ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokana na majina yao kutokuwapo katika orodha ya kurejea sokoni huko, serikali imesema uhakiki utafanyika upya.

Uhakiki huo ambao unatarajiwa kuanza Jumatatu ulitangazwa jana baada ya kikao kati yao na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alichoitisha kutokana na wafanyabiashara hao kugoma wakidai haki yao imepokwa.

Juzi Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, akizungumza na wafanyabiashara hao zaidi ya 900 waliokusanyika ofisi za CCM Lumumba, jijini, aliwaeleza kuhusu wito huo uliotolewa na Mkuu wa Mkoa.

Akizungumza na wafanyabiashara hao jana ofisini kwake Ilala baada ya kusikiliza hoja zao, Chalamila alimwagiza Meneja Mkuu wa Shirika la Masoko Kariakoo, Sigsibert Kaijage, kuwa kuanzia Jumatatu, wafanye uhakiki kwa mara nyingine ili wanaostahili wapate haki zao.

Chalamila alisisitiza kuwa kumeandaliwa utaratibu mpya katika soko hilo ambao unakwenda kuziba mianya ya madalali.

"Ndio maana tunafanya uhakiki, mfumo mpya tunaotaka katika Soko la Kariaokoo hauna nafasi kwa madalali, unakuta mtu mmoja anamiliki vizimba 10 na anapangisha wengine kwa gharama kubwa, hili hapana.

"Jambo ninalotaka mwondoke nalo hapa, utaratibu wa zamani hautakuwapo tena katika soko hili. Lazima ifike mahali tubadilike, lile ni soko la kimataifa na hata maduka hayatakiwi kuwa na vilemba. "Katibu Tawala wa Mkoa upo hapa na ile timu ipo hapa, ninataka uhakiki uende haraka ili tumwite Rais (Samia Suluhu Hassan) kuzindua soko," aliagiza Mkuu wa Mkoa.

Chalamila alikubali ombi la wafanyabiashara hao kushirikisha viongozi wao katika uhakiki huo wa mara ya pili na kuangalia namna ya kurejesha majina ya waliokuwapo awali ambao hawamo katika orodha iliyotangazwa.

Mkuu wa Mkoa huo pia alitahadharisha yeyote atakayejiingiza katika mfumo huo au kuleta ukanjanja atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. "Nyakati kama hizi zina upepo wa kisiasa, kuweni makini, madai haya yakibadilika kuwa mbinu za kisiasa hamtaambulia chochote, patachafuka! Kuna viongozi wanaotumia mianya hii ya kisiasa," alidai.

Chalamila alisema katika kuziba mianya ya madalali, gharama za maduka zitalingana na zile zinazozunguka katika maeneo hayo.

"Gharama zitaongezeka, soko limekarabatiwa vizuri na Rais Samia ameshalipa Sh. bilioni 20 kwa mkandarasi na limejengwa kwa Sh. bilioni 29," alisema. Mkuu wa Mkoa huyo pia aliagiza Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salam, Jumanne Murilo, aweke mipango thabiti ya kiuchunguzi itakayomulika mianya ya rushwa katika uhakiki utakaoanza Jumatatu.

Akitangaza utaratibu wa uhakiki huo, Kaijage alisema wafanyabiashara watajulishwa kupitia viongozi wao wa vitengo vyao.

Mfanyabiashara katika soko hilo, Yahya Hassan, alisema kitendo cha Chalamila kuwaita na kufanya nao mkutano na kukubali kufanya uhakiki tena, kitazaa matunda.

"Wakati wanahakiki mara ya kwanza wangewaita wale ambao waliona kuna shaka katika uhakiki wao, na kuwasikiliza tena kuona kwanini hawana vigezo na awali walikuwa wanafanya biashara," alisema.

Alidai kuwa nyuma ya pazia wanaona kuna rushwa inayotaka kufanyika au imeanza na kwamba kuna matajiri wakubwa na vigogo serikalini wameshaandaliwa tayari ili mfanyabiashara akishindwa kulipa apate nafasi.

"Tunaomba viongozi wetu wafuatishe kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan aliposema soko likikamilika waingie kwanza waliokuwapo, wakishaenea ndipo waanze kuingia wageni," alisema. Hassan pia aliomba serikali iongeze muda zaidi kwa wafanyabiashara wanaodaiwa kwa kuwa moto ulipotokea ulisababisha hasara kubwa kwao.

Ombi hilo linatokana na kauli ya Mkuu wa Mkoa huo aliyotoa mapema wiki hii kwamba wafanyabiashara waliokuwa na madeni kabla ya soko hilo kuungua wataingia baada kuyalipa.

Mfanyabiashara mwingine, Mariam Ngende, aliomba serikali iangalie wale waliorithi vizimba kutoka kwa walezi wao kwa kuwa katika orodha iliyotangazwa siku chache zilizopita, wapo wengi ambao hawajatambuliwa. "Wafanyabiashara tunajuana, kwahiyo serikali ingetumia viongozi wa wafanyabishara wakati wa kufanya uhakiki kwa kuwa wote tunafahamina, haya yote yasingetokea," alishauri. Abiba Hassan alidai wapo waliotoa mpaka Sh. milioni tano ili wapate sehemu ya kufanyia biashara na awali hawakuwapo.

"Wakati soko linaungua orodha ilikuwa inaonesha wafanyabiashara 1,662, lakini idadi iliyorudi imeonesha wapo 891, hii ndiyo sababu ya sisi kuandamana," alisema.

Hamza Mbaga, aliyekuwa anafanya biashara katika soko la wazi namba 45, alilalamikia jina lake kutokuwamo katika orodha iliyotolewa pamoja na kujaza fomu na kufanya uhakiki zaidi ya mara sita.

Usiku wa Julai 10, 2021, soko hilo liliungua, wafanyabiashara 224 wakipoteza bidhaa zao na serikali kutangaza kulifanyia ukarabati na kujenga jengo jipya la ghorofa nne juu na ghorofa mbili chini.




Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akizungumza katika kikao maalum na Rais wa Russia, Vladimir Putin jijini St. Petersburg, nchini humoi jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Tulia na Putin wateta mgogoro Russia, Ukraine

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Russia, Vladimir Putin jijini St. Petersburg, Russia kujadili namna bora ya kuimarisha amani duniani.

Mazungumzo hayo yaliyofanyika jana yaligusia pia mgogoro unaoendelea kati ya Russia na Ukraine.

Kupitia video fupi aliyorekodiwa, Dk. Tulia akiwa Russia alisema, "Kabla ya kuzungumza naye, tayari tulishazungumza na maspika wa nchi zote hizo mbili na sisi kama Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) tumezungumza naye kama kiongozi wa nchi.

"Tumezungumza naye katika sura ambayo tunaweza kuziweka pamoja nchi zote mbili na tutarajie kwamba, IPU itatengeneza fursa ya mabunge ya pande zote ili kuzungumzia amani katika maeneo yao ya utawala," alisema.

Dk. Tulia alisema wamezungumza pamoja na maspika hao mbele ya Rais Putin kwamba sasa wanaweza kupata nafasi ya kuzungumza na pande zote mbili kwa lengo la kuziweka pamoja kwa kuwa jambo hilo limezungumzwa kwa uzito.

"Na kwa kweli Mheshimiwa Rais, akiwapo pale basi sura inayokuja ni kwamba, tutarajie Umoja wa Mabunge Duniani utatengeneza sehemu fursa ya haya mabunge kuzungumzia amani katika eneo lao la utawala," alisema.

Kuhusu ziara hiyo, Dk. Tulia alisema ina malengo mawili, yakijumuisha kushiriki mkutano wa BRICS ambao ni muunganiko wa nchi 10 zenye malengo yanayofanana ambazo mabunge yao yanakutana hapo na

Alitaja lengo la pili IPU kuzungumzia mambo yanayotokea duniani hasa yanayohusu mizozo inayotishia amani.

"Russia ni moja ya nchi hizi za BRICS, na wakati huo huo niweze kusema yale ambayo ninafikiri yanaweza kutupeleka sehemu nzuri tukitumia fursa kama hii ya kukaa pamoja na kuzungumza kuhusu mizozo inayoendelea duniani.

"Kama tunavyofahamu Russia ni moja ya nchi zinazohusika na huu mzozo unaoendelea kati yake na Ukraine. Nimepata nafasi ya kuzungumza na viongozi na kesho (leo) tutaendelea kuzungumza na wengine. Mahsusi siku ya leo tumeonana na Rais wa Russia, Mheshimiwa Putin," alisema.

Dk. Tulia alisema kuzuru kwake Russia na malengo ya IPU ni kujaribu kutumia fursa au nafasi iliyopo; wabunge wanaweza kuitumia kwa kukaa pamoja kuzungumza namna wanavyoweza kuzishauri nchi zao kudumisha amani katika maeneo yao.

"Tumezungumza mambo mawili, moja kuhusu ushirikiano wa BRICS na Umoja wa Mabunge Duniani, tumezungumza mambo mengi tukiangazia maeneo ya mashirikiano kwa sababu Russia ni sehemu ya IPU kwa miaka 118 na imekuwa sehemu ya mabadiliko mengi ambayo yametokea katika umoja huu.

"Hata sasa ni sehemu ya IPU, tumepata nafasi ya kuzungumza namna tunaweza kutumia mabunge yetu kuhakikisha mzozo ulipo unafika mwisho.

"Jambo la pili, tumezungumzia kuhusu uhusiano kati ya Tanzania na Urusi, katika eneo hili tumeangazia mambo ya ushirikiano ambayo yapo katika eneo la kiuchumi, kibiashara na nishati," alisema.

Dk. Tulia alisema hayo yote wameyazungumza katika sura ya viongozi wa kitaifa waliopata nafasi ya kwenda Russia, mengine walishaanza kuzungumza.

"Tuliyozungumza yanahitaji ufuatiliaji, pengine nisingependa kuyasema, lakini kwa ujumla Watanznaia wafahamu tumepata nafasi ya kuzungumza kwanza yanayohusu Umoja wa Mabunge Duniani mimi kama Rais wa IPU, tumezungumza yanayohusu ushirikiano kati ya nchi hizi mbili.

"Yapo ambayo mimi kama Spika wa Bunge niweze kuyafuatilia na kuishauri serikali juu ya uamuzi wa mambo hayo ambayo tumeyazungumza.

"Pia kuliongoza Bunge katika kusimamia serikali yale mambo ambayo serikali imeshaingia na nchi nyingine," alifafanua.

HABARI KITAIFA

# Uamuzi kumwengua Mwabukusi wazidi kuchafua hali ya hewa TLS

**Na Restuta James**

KUKATWA jina la Boniface Mwabukusi katika orodha ya wagombea urais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kunazidi kupingwa:

Jumuiya ya Mawakili Vijana nayo imeungana na wadau wengine wanaopinga uamuzi huo, ikitoa mapendekezo saba likiwamo la kutaka wajumbe wa Kamati ya Rufani ya Uchaguzi wajiuzulu.

Taarifa iliyotolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo iliyomo ndani ya TLS, Edward Heche, ilibainisha kuwa uamuzi wa Kamati ya Rufani ya Uchaguzi kumwengua Mwabukusi umetolewa kinyume cha Kanuni ya 50(2)(a) na (b) ya uchaguzi wa TLS ya Mwaka 2022.

"Ili kulinda heshima, hadhi na haiba ya mawakili na umadhubuti wa TLS, tunatoa wito kwa mawakili vijana kwamba, tumuunge mkono Wakili Mwabukusi katika jitihada za kisheria ili kurejesha jina lake katika kapu la uchaguzi.

"Tusishiriki mchakato wowote wa uchaguzi wa TLS kuanzia sasa hadi jina la Wakili Mwabukusi na wenzake yatakaporejeshwa. Lengo ni kulinda mawanda ya ushiriki na ushindani ndani ya chama chetu," alisema Heche.

Aliwataka mawakili vijana kutoshiriki mchakato wowote wa uchaguzi wa TLS kuanzia sasa hadi jina la Wakili Mwabukusi na wenzake yatakaporejeshwa, ili kuweka mazingira ya uchaguzi wenye ushindani.

"Sisi kama Jumuiya ya Vijana, tunatoa wito kwa Baraza la Uongozi kuingilia kati na kunusuru mchakato huu ikiwamo kuiondoa na kuifuta Tume ya Rufani ya Uchaguzi... baraza likutane kwa dharura kuangalia madhara ya mgawanyiko uliojitokeza na kurejesha katika mchakato wa uchaguzi jina la Wakili Mwabukusi na wawakili wengine wote wenye sifa," alisema.

Pendekezo lingine la jumuiya hiyo ni Baraza la Uongozi kuchunguza wajumbe wa Kamati ya Rufaa chini ya tume huru kupitia mawakili waadilifu na kuchukua hatua za kinidhamu ikiwamo kuwashtaki kutokana na alichodai kuwa kukiuka maadili ya taaluma ya sheria.

Vilevile, alisema wanataka majina ya mawakili wenye sifa yaliyoenguliwa yarejeshwe mara moja.

Jumuiya hiyo pia imeomba Mkutano Mkuu wa TLS uliopangwa kufanyika jijini Dodoma Agosti 1-3 mwaka huu, upitishe azimio kwa kutoa tamko kwamba uamuzi wa kumwengua Wakili Mwabukusi umefanywa katika namna ambayo imekiuka sheria za uchaguzi, maadili ya taaluma ya sheria na mantiki za kisheria (legal logic) na akili ya kawaida (common sense).

"Mkutano Mkuu upitishe azimio la kuwataka wajumbe wote wa Kamati ya Rufani ya Uchaguzi ijiuzulu ndani ya saa 48 baada kupitishwa azimio isipokuwa Wakili Mwandamizi Nakazael Tenga ambaye alikataa uamuzi tajwa," alisema Heche.

Alipendekeza kuwa ikiwa wajumbe hao hawatajiuzulu ndani ya saa 48, Mkutano Mkuu upitishe azimio la kulielekeza Baraza la Uongozi livunje Kamati ya Rufani ya Uchaguzi na kuwafuta kazi wajumbe wote wa Kamati ya Uchaguzi isipokuwa Wakili Tenga.

"Mkutano Mkuu upitishe azimio la kuielekeza Kamati ya Uchaguzi ifute notisi ya uchaguzi mkuu na mchakato uanze upya na uchaguzi mkuu ufanyike katika Mkutano Mkuu ujao wa mwaka 2025.

"Mkutano Mkuu upitishe azimio kwamba Kamati ya Maadili ya Kitaifa iwachukulie hatua za kinidhamu wajumbe wote wa Kamati ya Rufani ya Uchaguzi kwa kukiuka maadili ya taaluma ya sheria kwa namna ambayo imechafua hadhi, heshima na taswira ya chama chetu," alipendekeza.

Heche pia alisema, "Hatutakubali uchaguzi ufanyike bila haki kuonekana imetendeka kwa Wakili Mwabukusi na wenzake. Hatutakubali kwa namna yoyote watu wachache kuharibu na kuua hadhi ya uwakili na taswira ya chama chetu kwa sababu zao binafsi."

Mwenyekiti huyo alisema kumwengua Wakili Mwabukusi na baadhi ya mawakili ni kuminya wigo wa ushiriki wa mawakili katika uamuzi wa chama chao na ushindani katika uchaguzi.

"Mwabukusi ameenguliwa kwa nia ovu kwa kuwa sababu zilizotajwa na Kamati ya Rufani hazina mashiko, ni za kubashiri, za kibaguzi na hazina msingi katika sheria na haki... ni dhihaka kwa tasnia ya uwakili na taaluma ya sheria," alidai.

Heche alisema mawakili wanapaswa kuzingatia sheria, weledi na maadili katika kufanya uamuzi na kwamba kwenda kinyume cha msingi huo ni kuchafua taswira ya TLS.

Kwa mujibu wa Heche, mawakili Omari Aziza Msangi, Irene Mwakyusa na Steven Kitale wameenguliwa kwa hila kwa kuwa ni miongoni mwa wanaomwunga mkono Wakili Mwabukusi.

"Sisi kama Jumuiya ya Vijana ndani ya TLS, hatutakubali uchaguzi huu ufanyike bila haki kuonekana imetendeka... hatutakubali kwa namna yoyote kuacha watu wachache kwa maslahi yao binafsi waharibu na kuua hadhi ya uwakili na taswira yaTLS kwa maslahi binafsi," alisema.

Wakili Mwabukusi alienguliwa kuwania urais wa TLS kwa kile kilichoelezwa ni kwa maslahi ya umma kwa madai ya utovu wa nidhamu.

Baada ya kuenguliwa kwa wakili huyo, wagombea wanaochuana kuwania urais wa TLS hivi sasa ni Kapteni Ibrahim Bendera, Emmanuel Muga, Revocatus Kuuli, Paul Kaunda na Sweetbert Nkuba.

Uchaguzi wa TLS umepangwa kufanyika jijini Dodoma Agosti 2 mwaka huu.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Alban Kihulla (kulia), akifafanua jambo kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (katikati) alipotembelea kituo cha kupimia malori ya mafuta cha Misugusugu, Kibaha mkoani Pwani jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa wizara hiyo, Exaud Kigahe. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri Jafo afichua wauza nyama 'wanavyowapiga' wateja buchani

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo amefichua namna wauza nyama buchani wanavyocheza na mizani na kuwaibia wateja wao kwa kuwawekea vipimo visivyo sahihi.

Alibainisha mbinu hizo jana alipotembelea kituo cha kupimia ujazo wa malori cha Wakala wa Vipimo (WMA) cha Misugusugu, mkoani Pwani, akiwa ameambatana na Naibu Waziri wake, Exaud Kigahe na Naibu Katibu Mkuu wizarani, Balozi Dk. John Simbachawene.

"Ile mizani ya zamani yenye sufuria upande mmoja na jiwe kwingine kila ukiondoka unakuta kaweka jiwe la ujazo wowote, hawezi kuuacha mzani ukiwa bila jiwe.

"Ukiingia buchani anakuuliza unataka kilo ngapi, ukisema tu anatoa jiwe alilokuwa ameweka anaweka la ujazo unaotaka wewe, ule ni ujanjaujanja tu wa kukuibia.

"Anaweka jiwe muda wote kwa sababu anajua lisipokuwapo mizani haiwezi kuwa sawa, kwahiyo mteja anaweza kushtukia kwa sababu akitoa jiwe tu mzani unaangukia kwenye lile sufuria kubwa upande mwingine. Kwahiyo, unapimiwa kilo moja wakati mwingine robo nzima imeibiwa.

"Sijui kama wenzangu mnayaona haya lakini inawezekana wengine ni wa mboga nane hamjawahi kuishi maisha ya uswahilini, hivyo hamwezi kuelewa hiki ninachosema, lakini ndiyo hali yenyewe," alisema Waziri Jafo.

Alisema wapo baadhi ya wafanyabaishara ambao wamekuwa wanatumia mbinu zingine za kuwaibia wateja ikiwamo ya kukandamiza mizani kwa kutumia kisu, wengine wakitumia sumaku.

Alisema WMA ina kazi kubwa ya kupambana na wizi huo, akiwataka viongozi wake kushirikisha maofisa biashara wa mikoa na wilaya kuwatafuta na kuwachukulia hatua za kisheria wote wanaohusika na vitendo hivyo.

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo alielekeza watendaji walio chini yake kumaliza hujuma zinazofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wanaopunguza ujazo wa mifuko ya saruji.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu kupungua kwa ujazo wa mifuko hiyo ya saruji ambayo inapotoka kiwandani inakuwa na ujazo sahihi wa kilo 50, lakini inafika kwa wateja ikiwa na wastani wa kilo 40 au 45.

"Inawezekana ikawa ni kazi kubwa, lakini sisi ndiyo tumepewa wajibu wa kuhakikisha kunakuwa na vipimo sahihi, mtendaji mkuu na timu yako mnapaswa kusimamia kuhakikisha hujuma hizi zinakomeshwa," aliagiza Waziri Jafo.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Exaud Kigahe alimpongeza Dk. Jafo kwa kuanza kazi kwa kasi baada ya kuapishwa hivi karibuni na kumwahidi kuwa atampa ushirikiano katika utendaji kazi wake.

Alisema taasisi nyingi zilizo chini ya wizara hiyo zinafanya kazi ya kuweka mazingira mazuri ya wenye viwanda na biashara kustawi na kulinda ushindani kwenye biashara na walaji wa mwisho ili wanaouza wasiibiwe na wale wanaonunua wasiibiwe.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla alisema wamepokea maelekezo yote yaliyotolewa na waziri na kuahidi kuyafanyia kazi katika muda uliopangwa.

Kihulla alieleza kuwa WMA kupitia kituo hicho cha Misugusugu, ina uwezo wa kuhakiki mita za umeme, dira za maji na magari yanayotumika kusafirisha vimiminika.

# TEF, MISA-TAN walaani mwandishi kushambuliwa

**Na Restuta James**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) limelaani tukio la kushambuliwa Mhariri wa Habari za Biashara wa gazeti The Guardian, Dickson Ng'hily na kuonya kwamba kushambulia mwandishi wa habari kunachafua taswira ya nchi kimataifa.

Ng'hily ambaye pia ni Mkuu wa Dawati la Nipashe Digital, anadaiwa kujeruhiwa Jumatano ya juma hili kwa kupigwa na walimu wa Shule ya Msingi Kwembe, Manispaa ya Ubungo, alipopiga picha wanafunzi waliokuwa wanasoma chini ya mti.

Taarifa ya Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, ilieleza kuwa jukwaa hilo litashirikiana na mwandishi huyo kuhakikisha wahusika wanachukuliwa hatua stahiki ikiwamo kulipa gharama ya hasara waliyomsababishia.

Balile katika taarifa hiyo alisema kitendo kilichofanywa na walimu hao ni jinai na hujuma dhidi ya juhudi anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kurejesha uhuru wa vyombo vya habari nchini kwa kuzuia waandishi kukamatwa, kupigwa, kuzuiwa kufanya kazi na kunyanyaswa.

"Ameyazuia tangu alipoingia madarakani Machi 19, 2021, hali iliyoipandisha Tanzania katika viwango ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani kwa nafasi 46, yaani kutoka nafasi ya 143 hadi nafasi ya 97.

"Vitendo vya aina hii vikiendelea nchi yetu itashuka tena na kuathiri kuaminika kwake mbele ya jamii ya kimataifa, hivyo kukimbiza wawekezaji," alisema.

Balile aliongeza kuwa, "TEF tunalaani kwa nguvu zote kitendo hiki na tunavisihi vyombo vya dola vimpe ushirikiano wa kutosha Mwandishi Ng'hily, ambaye tayari ameanza mchakato wa kufungua kesi ya jinai dhidi ya wote waliohusika katika kadhia hii."

Alikumbusha kwamba uandishi wa habari chini ya Kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Huduma za Habari (MSA) ya Mwaka 2016, kama ilivyorekebishwa mwaka 2023, ni taaluma inayotambulika kama taaluma nyingine nchini na kwamba utetezi wa Wilaya ya Ubungo 'kumweka mwandishi chini ya ulinzi kujiridhisha kama ana kibali cha kupiga picha' ni mwendelezo wa jinai sawa na walivyofanya walimu waliompiga Ng'hily.

"Tunajiuliza ukaguzi huo walitaka kuufanya kwa kutumia sheria ipi au walipata wapi mamlaka hayo? Nani kawaambia mwandishi wa habari akikuta tukio linaendelea anapaswa kuandika barua ya maombi ya kibali cha kupiga picha, kiidhinishwe kwanza ndipo arudi kupiga picha?

"Duniani kote, mwandishi akikuta tukio anapiga picha kwanza kisha anawatafuta wahusika kupata ufafanuzi. Kwanini Wilaya ya Ubungo na walimu wa Shule ya Msingi Kwembe wanataka kutunga kanuni mpya isiyokidhi vigezo vya uandishi wa habari?" alihoji.

**MISA-TAN**

Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA TANZANIA) pia imekemea tukio hilo kwa maelezo kuwa kujichukulia sheria mkononi ni kinyume cha sheria.

"Katika dunia ya ukuaji wa teknolojia, kuzuia mwandishi wa habari kupiga picha ni sawa na kuzuia mabadiliko kwa kuwa picha zinaweza kupigwa kwa namna nyingi bila mhusika kufika eneo husika... tunakemea uamuzi wowote wa kujichukulia sheria," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

"Licha ya mwandishi huyo kujitambulisha na kuonesha vitambulisho vyake, bado waliendelea kumshambulia kama mhalifu. Kitendo hiki hakikubaliki kwa kuwa kinakwenda kinyume cha sheria na kusigina uhuru wa kupata taarifa na uhuru wa vyombo vya habari."

Inadaiwa kuwa baada ya kumshambulia, walimu walikwenda mbali zaidi kwa kumpeleka mwandishi huyo ofisi za serikali ya mtaa na baadaye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ubungo.

Pia inadaiwa kuwa pamoja na kipigo, walimu hao na wanafunzi waliharibu vifaa vyake vya kazi ikiwamo simu ya mkononi waliyoipasua kioo, wakamnyang'anya na kufuta picha alizopiga.

UDANGANYIFU VYUONI

# Wazazi waangua kilio ofisini kwa waziri

## -Masharti magumu utetezi wa tasnifu za PhD

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (pichani) ameweka wazi kuwa watu wengi wamekuwa wanafika ofisini kwake wakiomba watoto wao warejeshwe vyuoni baada ya kufukuzwa kutokana na kufanya udanganyifu.

Prof. Mkenda aliyasema hayo jana wakati akizungumzia udanganyifu vyuoni ambao umeripotiwa hivi karibuni na vyombo vya habari baada ya kikao chake na makamishna.

"Mimi nina watu chungu nzima ofisini, wazazi wao wanaomba kwa waziri, 'tunaomba mtoto wetu arudi alifukuzwa, ameonewa'. Ninachofanya mimi ni kurudi katika utaratibu wa chuo kuuliza nini kimetokea.

"Unakuta utaratibu ulifanyika seneti, hatimaye imemfukuza amepewa muda wa kukata rufani hajakata au amekata.

"Lakini kama waziri nimekataa katakata kuingilia mamlaka ya vyuo vikuu wanapochukua hatua kama hizo kwa kuwa tunalinda suala la mitihani," alisema.

Prof. Mkenda alihimiza vyuo vikuu viendelee kufanya hivyo na hata jitihada zilizofanyika hivi karibuni Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT) kwa waliojaribu kufanyiwa mitihani, alisema ni kati ya jitihada ambazo zinaendelea kwa vyuo vyote.

Waziri huyo alisema ili mtu afanye mtihani, ni lazima aende na kitambulisho chake na kukaa mezani na sura ya mhusika ionekane.

Pia alikumbusha kuwa ni marufuku mtu kuingia na simu katika chumba cha mtihani na anayekutwa hufukuzwa chuoni.

"Baadhi ya watu wanalalamika tumekuwa hatutendi haki, lakini ndio ukweli wenyewe. Unaweza ukatumia simu kuja na majibu kwenye mtihani. Majaribio ya udanganyifu yataendelea kuwapo kwa sababu yapo dunia nzima na sisi tutaendelea kuwabana.

"Ninatoa wito kwa wanafunzi wote unaweza kufanya kitu kidogo na una uwezo mkubwa, lakini utafukuzwa na vyuo vingi vikikufukuza huruhusiwi kurudi mara moja, unapewa muda mrefu kukaa nyumbani. Kama ulifukuzwa mwaka wa tatu utarudia mwaka wa kwanza," alionya.

Prof. Mkenda alisisitiza kwamba kila tuhuma wanapopata huzifanyia kazi na kuomba yeyote anayehisi kuna suala analifahamu, alipeleke Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili kufanyiwa kazi.

"Tuhuma hizi zinavyosemwa zinaweza kusababisha watu wakadhani hali ya vyuo vikuu vyetu ni mbaya sana.

"Ninawahikikishia Watanzania bado vyuo vikuu vyetu vinazingatia maadili hasa katika masuala ya mitihani na weledi kuhakikisha tunatoa shahada kwa mujibu wa taratibu zinazokubalika katika taaluma zetu," alisema.

Alisema udanganyifu upo duniani lakini kikubwa ni mbinu zinazotumika kuuzuia.

"Kuna msemo unasema, 'adhaniane amesimama, aangalie asianguke', kila tuhuma zinaposemwa tunachukulia ni jambo kubwa na zito," alisema.

Prof. Mkenda alitolea mfano mitihani ya darasa la nne na la saba inayosimamiwa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), akisema licha ya mashinikizo waliyopata, hatua zilichukuliwa zikiwamo zinazoumiza maslahi ya wawekezaji katika sekta ya elimu.

"Tunaamini suala la udanganyifu katika mitihani madhara ni makubwa, kwanza linaondoa usawa na haki, linaondoa weledi halafu akapewa majukumu kama udaktari na kwenda kuhudumia umma.

"Tukiruhusu udanganyifu ngazi zote za elimu ni kama vile kulea na kufundisha rushwa kwa wanafunzi wetu. Ndio maana baadhi ya hatua tumechukua, lakini watu wanalaumu, tunaomba umma utuelewe; tunafanya hivyo ili kulinda mfumo wa elimu," alisema.

Prof. Mkenda alisema katika sekta ya elimu wameleta mabadiliko ya sheria ili kubana zaidi wanaofanya udanganyifu kwenye mitihani, hivi karibuni wamehukumiwa baadhi ya watu waliofanya hivyo.

Kuhusu vyuo vikuu, alisema vina kanuni za kusimamia mitihani ambazo hata TCU inazifahamu na mtu anapokamatwa kwenye udanganyifu wa mitihani adhabu ni kufukuzwa chuo moja kwa moja mara baada ya kuthibitishwa kwa tukio husika.

Prof. Mkenda alisema kuna gazeti limeandika kuhusu utaratibu wa wanafunzi kuhonga ili matokeo yaliyoingizwa katika mfumo wa TEHAMA yabadilishwe.

Alisema habari hiyo imetaja jina la mwanafunzi na aliyehusika kubadilisha matokeo hayo, hivyo akamwagiza Katibu Mkuu kuunda kamati huru kuchunguza kwa kushirikiana na Idara ya Usalama wa Taifa na wataalamu wa TEHAMA.

"Waliingia na kuangalia mfumo wote wa TEHAMA. Uzuri mabadiliko yoyote kwenye TEHAMA mabadiliko yoyote



yanaonesha mtu aliingia saa ngapi na iliingizwa alama ipi na kama kuna mabadiliko utaona.

"Tulichunguza na kugundua si kweli. Nadhani kwenye chuo hicho kuna mnyukano tu, kuna mtu au watu wanajua Makamu Mkuu wa Chuo anastaafu hivi karibuni, basi kuna kuchafuana au dalili katika kinyang'anyiro cha kuchukua nafasi watu wanachafuana," alisema.

Prof. Mkenda alisema wamekubaliana na Katibu Mkuu aiombe Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ichukue chuo hicho kama mfano kwenda kufanya uchunguzi wa kisayansi wa matokeo yote yaliyoingizwa katika TEHAMA na kama yakibadilika, ijulikane nani anayefanya hivyo.

Waziri huyo alisema kuna wakati alipata tuhuma za mtu kuondolewa chuoni katika chuo kikuu kimoja kwa kufeli. Badala ya kukata rufani, alitumia muda huo kwenda kwa watu wazito ambao walikuwa wakimpigia waziri simu wakihoji kwanini ameondolewa na anadai amenyanyaswa.

Hata alipoambiwa akate rufani licha ya muda wake kuisha, alikataa na anachokitaka ni kutumia watu wazito kutoka nje ya mfumo wa elimu kumwombea.

"Hii haitakaa itokee vyuo vikuu tunavisimamia lakini hatuviingilii, kuna utaratibu wa kukata rufani katika seneti kama umehisi umeonewa au ukaja kwa waziri ili kujadiliana na chuo kuona namna ya kuhakiki.

"Huwezi ukawa umefeli mtihani hutaki kufuata taratibu za rufani, unatafuta mtu maarufu unasema, 'ninaomba kaniombee kwa waziri, wale wenye ushahidi wa udanganyifu leteni tutafanyia kazi," alisema.

Pia alisema waandishi wa habari rukhsa kuandika matukio hayo, lakini wanapoombwa ushahidi japo wa jina chuo bila kumtaja mtoa taarifa, wasiache kuutoa ili ufanyiwe kazi.

Kuhusu wanaochukua Shahada ya Uzamivu (PhD), waziri huyo alisema wameshakubaliana ikiwa ni mwaka sasa; kabla ya kuipata lazima wasimame mebele ya kamati na kupigwa maswali na wasipofaulu wakati wa kujitetea wamefeli.

"Unaweza kufeli na kuondolewa kabisa au hujafaulu vizuri unaambiwa kutengeneza kazi yako vizuri. Utetezi wa PhD Tanzania lazima ufanyike hadharani na TCU imeshaweka kama kanuni.

"Itatangaza mfano, Adolf Mkenda Septemba 3, mwaka huu, anayo tasnifu ya PhD inayohusu mambo ya samaki na uchumi, atafanya utetezi saa nane kwenye ukumbi fulani, mtu yeyote anayetaka kuangalia atapata fursa hii," alisema.

Vilevile, waziri huyo alisema kwa wanaochukua shahada ya uzamili bila kufanya mitihani ya kawaida darasani, utetezi wao utakuwa wa hadharani.

Alisema lazima mwanafunzi ahakikishe kazi aliyoandika ni yake, hajachukua ya mtu na endapo atafanya hivyo ikigundulika, wamekubaliana mhadhiri aliyepitisha andiko la utafiti na mwanafunzi watachukuliwa hatua.

"Hata tukikuta kuna andiko la utafiti chuoni kwako tukagundua hukufanya uhakiki na kubaini si kazi ya mwanafunzi husika, chuo tutakitangaza kimeruhusu hilo na tutataka ifutwe na yule mtu anyang'anywe certificate (cheti)," alisema.

# Ajali ilivyoua mapadri, bruda

**Na Romana Mallya**

WATU watatu, wakiwamo mapadri wawili wa Kanisa Katoliki, wamefariki dunia kutokana na ajali mkoani Lindi.

Imeelezwa na Jeshi la Polisi kuwa watatu hao walifikwa na umauti jana baada ya gari walilokuwa wanasafiria kugonga shimo barabarani na kupoteza mwelekeo kisha kutumbukia korongoni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi John Imori, alisema ajali hiyo ilitokea saa 12 asubuhi eneo la Mtualonga, barabara ya Masasi-Mnazi Mmoja, Halmashauri ya Mtama.

Kamanda Imori alisema ajali hiyo ilihusisha gari namba T 139 DZZ aina ya Mitsubishi Outlander lililokuwa linatoka Ndanda, Mtwara kwenda Dar es Salaam.

Kamanda huyo alitaja mapadri waliofariki dunia ni Cornelius Modoe (55), mkazi wa mkoani Dar es Salaam; Pius Boa (51), mkazi wa Lushoto, mkoani Tanga na Haphymark Mkenda (51) ambaye ni bruda, mkazi wa Dar es Salaam.

Alisema katika ajali hiyo, watu wengine wawili wamejeruhiwa ambao ni Bruda Edmond Kimario, mkazi wa Njombe na Mwalimu wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Ndanda, Juma Makota, mkazi wa Ndanda.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva kushindwa kumudu gari baada ya kugonga shimo katika barabara hiyo na kupoteza mwelekeo na kupinduka na kutumbukia katika korongo. Majeruhi walipelekwa Hospitali ya Misheni Ndanda pamoja na miili hiyo.

Kamanda huyo alitoa wito kwa madereva kuchukua tahadhari kwa kuwa barabara hiyo baada ya mvua kubwa kunyesha imekuwa na mashimo mengi, hivyo kuzingatia sheria za usalama barabarani ni jambo la msingi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wawakilishi wa Tanzania jiandaeni vizuri CAF

**SHIRIKISHO** la soka Afrika (CAF) lilichezesha droo ya timu zitakazokutana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho ambapo wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo tayari wamewafahamu wapinzani wao.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, mabingwa wa soka Tanzania, Yanga wenyewe wataumana na Mabingwa wa Burundi, Vital'O Club huku Azam FC ikipangwa kucheza na APR ya Rwanda ambapo Yanga wataanzia ugenini huku Azam wakianzia nyumbani kati ya Agosti 16 na 18.

Katika droo hiyo iliyochezeshwa Makao Makuu ya CAF, Cairo, Misri, timu zote za Tanzania zitaanzia hatua ya awali isipokuwa Simba inayoshiriki Kombe la Shirikisho itaanzia hatua ya kwanza kwa kusubiri mshindi kwenye mchezo kati ya Uhamiaji FC ya Zanzibar na mwakilishi kutoka Libya ambaye bado hajapatikana.

Katika kombe hilo, Coastal Union yenyewe itacheza na FC Bravos do Maquis ya Angola katika hatua ya awali.

Mwakilishi mwingine wa Zanzibar michuano hiyo, JKU inayoshiriki Ligi ya mabingwa yenyewe imepangwa kucheza na Pyramids ya Misri na mshindi katika mchezo huo atacheza na mshindi kati ya Azam FC na APR.

Michezo ya marudiano imepangwa kuchezwa kati ya Agosti 23 mpaka Agosti 25.

Kwa ratiba hiyo, ni kwamba Yanga na Azam zimedondokea kwenye timu za Ukanda wa Afrika Mashariki na wanachama wa CECAFA.

Endapo Yanga atafanikiwa kumuondoa kwenye michuano hiyo Vital'O, ataumana na mshindi kati ya Villa SC ya Uganda watakaocheza na Commercial Sports ya Ethiopia.

Wakati droo hiyo inatoka tayari timu za Tanzania zimeshaanza maandalizi ya kuelekea kwenye msimu mpya, ambapo Yanga ilianza mazoezi kwenye ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam, chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, ikitarajia pia kwenda nchini Afrika Kusini kucheza mechi ya Kombe la Toyota dhidi ya Kaizer Chiefs utakaopigwa Julai 28.

Azam FC yenyewe iko Zanzibar na leo inatarajiwa kukipiga na Zimamoto kwenye mchezo wa kirafiki, huku ikiwa kwenye maandalizi ya kuelekea nchini Morocco kuweka kambi.

Simba ambayo itasubiri hadi Septemba kucheza michuano hiyo ya CAF, nayo imeanza maandalizi ambapo tayari ipo nchini Misri kwenye jiji la Ismailia ikijifua kwa ajili ya michuano hiyo na Ligi Kuu.


Nipashe tunasema kwamba, Wawakilishi wa Tanzania wanatakiwa kutumia nafasi yao vizuri ya mandalizi kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao ili kuweza kupaata matokeo mzuri na hatimaye kufuzu hatua inayofuata.

Kama timu hizo zitakuwa zimaejipanga vizuri kama ambavyo viongozi wake wanavyojinasibu, basi Tanzania inaweza kuhushudia wawakilishi wao wakiisonga mbele katika hatua kubwa zaidi ya mashindano hayo.

Sisi rai yetu ni kwamba sasa ni wakati muhimu kwa timu zote kufanya mazoezi kwa bidii ili kuhakikisha wanaiwakilisha vyema Tanzania kimataifa.

Haitosahi tu kufuzu hatua inayofuata, bali ni kuhakikisha timu zinafika mbali zaidi na ikiwezekana hata kubeba ubingwa wa mashindano waliyopo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Viwanja vya soka viwe mtoko wa familia, isiwe kama adhabu

**NILIKUWEPO** kwenye Uwanja wa Manispaa ya Kinondoni, Mwenge jijini Dar es Salaam siku ya ufunguzi. Kulikuwa na mambo mawili, ufunguzi wa uwanja wenyewe pamoja na Kombe la Dar Port Kagame.

Moja kati ya mechi nilizoshuhudia katikati ya wiki hii ni ile ya Coastal Union dhidi ya Dekedaha FC ya Somalia, ikishinda kwa bao 1-0.

Ukiachalia mbali soka, lakini kilichonifurahisha ni jinsi mazingira ya watu waliokuwepo uwanjani humo.

Kama inavyojulikana Mwenge, licha ya kwanza kwa sasa ni eneo la Kibiashara, lakini pia ni lenye makazi ya watu kama ilivyokuwa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Watu waliokuwemo humo, wengi wao walikuwa ni wanawake wa umri mbalimbali, kuanzia wasichana wadogo mpaka akinamama.

Tena wengine walikuwa wamebeba watoto mgongoni na wengine walikuwa wamewashikilia na walikuwa bize kutazama soka.

Niligundua kuwa baadhi yao walikuwa hata hawajui timu gani zinacheza, lakini kwa sababu kuna mechi na mazingira mapya ya uwanja, walijongea.

Kilichoonekana ni kwamba pamoja na baadhi ya wafanyabiashara ya soko la Mwenge na maduka, lakini wengine hasa kinadada na kinamama walikuwa ni majirani wa eneo hilo.

Walikusanya familia na kusogea hapo kama mtoko. Ilionekana kama sikukuu hivi, kwani ndani mle mlikuwa mnauzwa vitu mbalimbali, viburudisho na vitafunwa, hivyo watu walionekana kuinjoi sana. Niwapongeze sana viongozi wa Manispaa ya Kinondoni kwa kuujenga uwanja huo hasa maeneo ya kibiashara yaliyochanganyikana na makazi ya watu, kwani wameupeleka eneo la watu kabisa tofauti kama wangeujenga sehemu nyingine.

Uwanja huo ndiyo utakuwa uwanja wa nyumbani wa timu ya KMC, lakini pia hata klabu zingine zina fursa ya kuomba kuutumia.

Nikitoka hapo, nilipongeze pia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kwa kuamua kuukarabati uwanja wao wa Meja Jenerali Isamuhyo.

Wenyewe wanasema, pamoja na mambo mengine ya 'pitch', wanazungusha viti ili mashabiki wasipate tabu ya kusimama.

JKT na KMC wameonyesha dira kubwa kwa kujenga viwanja, hivyo kuwapa tamaa klabu zingine kufanya hivyo.

Tunahitaji viwanja vya aina hiyo hata kama ni vidogo, lakini viwe vingi kwa ajili ya kupunguza msongamano wa mechi mbalimbali za Ligi Kuu na michuano mingine.

Pamoja na yote bado nazikumbusha mamlaka za soka na wenye viwanja nchini kutengeneza mazingira ya kuvifanya kuwa rafiki kwa watazamaji wasijione kama wapo polisi au mahakamani.

Sina maana kuwa sehemu hizo ni mbaya, au zina matatizo, la hasha, ila haiondoi ukweli kuwa ndiyo sehemu ambazo watu wanakaa kwa uangalifu, heshima, adabu, woga na wasiwasi pia.

Na ndiyo sehemu ambazo raia huwa hawapendi sana kwenda, akifanya hivyo ujue amelazimika kweli, anakwenda kutafuta hali yake, au amepelekwa.

Mpirani hakutaki kuwa hivyo, badala yake ni sehemu ya burudani kama mtu aliyekuwa baa, disco, au kwenye ukumbi wa dansi au sherehe.

Kwa maana hiyo wamiliki wa viwanja, serikali na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), kuangalia na kutengeneza mazingira ya watu kupenda kwenda uwanjani, kama wanavyofurahia kwenda harusini, au kutazama ngoma, au shoo yoyote. Zama za mtu akitaka kwenda uwanjani, anafikiria usalama, purukushani, mbwa mlangoni, njaa, kiu, zimepitwa na wakati.

Siku hizi tunaona hata akinamama na watoto wanakwenda uwanjani, hivyo wanapaswa kulindwa ili waendelee kuja na waongezeke.

Imefika wakati sasa viwanja vyetu kuwa kama vya nje, ambapo kuwe na vitafunwa, maji kwenye glasi nyepesi kuepuka warusha chupa, vyakula, vinywaji, kama vile watu wako 'pikniki' na si vitu hivyo kupatikana eneo la VIP tu.

Kwa kipindi hiki ambacho mashabiki wamekuwa wachache viwanjani, mazingira kama haya yatavutia mashabiki wengi ambao baadhi wanaweza kuingia si kutazama soka tu, badala yake kuinjoi kama mtoko hivi, kutokana na huduma zinazopatikana viwanjani.

**HABARI KITAIFA**

# Wapata dawa kamatakamata katika maegesho yasiyo rasmi

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetangaza mwarobaini wa kamatakamata ya magari katika maegesho yasiyo rasmi, ikilenga pia kudhibiti vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya watu wasio waadilifu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, katika mkutano wa hadhara jijini juzi ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya siku saba ya Katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM, Amos Makalla, alisema haiwezekani watu wakamatwe.

Chalamila alisema mkoani humo kuna 'ugonjwa' wa kukamatakamata watu wanaoegesha gari sehemu isiyo sahihi (wrong parking).

"Ukienda jiji, wrong parking (maegesho yasiyo sahihi) ukienda wapi wrong parking, sasa tumesema hivi na Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya wapo hapa, wanasikia na meya ananisikiliza, tumesema huwezi kukamata watu kama hujawaonesha sehemu sahihi ya maegesho," alisonya.

Chalamila alisema miongoni mwa maeneo waliyotoa maelekezo ni pamoja na kwenye masoko, wakiwataka viongozi wawekeze katika maegesho ili "yale mambo ya mtu anakwenda anaviziavizia na katumbo kake anataka rushwa ipo siku (mtu huyo) atapigwa vibao."

Aliongeza, "Lazima katika ujenzi huu kunakuwa na maegesho, unakuwa mradi wa kudumu wa Jiji la Dar es Salaam ili watu wa namna hii wakome na iwe mwisho.

Yahya Mohamed, mkazi wa Buguruni, jijini, alipongeza uamuzi wa Chalamila, akisema uwekezaji katika ujenzi wa maegesho utasaidia serikali kupata mapato na kuondoa pia usumbufu kwa wenye magari.

Katika mkutano huo, Chalamila pia alizungumzia changamoto ya majitaka iliyoko maeneo tofauti mkoani humo ikiwamo yanayotiririka katika makazi ya watu, akisema kuwa licha ya wananchi kulipia huduma hiyo, imegeuka kuwa kero kwao.

"Majitaka haya hapo mbele (Mchikichini) ukienda yapo yanajitokeatokea tu mtu wa DAWASA njoo hapa," alimwita jukwaani.

Katika majibu yake, Mwakilishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), aliwaeleza wananchi kwamba, wamejipanga kuboresha miundombinu hiyo mkoani humo ili huduma hiyo iwe salama kwa watumiaji.

Pamoja na majibu hayo, Chalamila alisema, "Majitaka yapo mbele hapo (Mchikichini) leo hii ukienda kunatiririka haja kubwa, hali si nzuri, huo ndio ukweli.

Chalamila aliitaka DAWASA ikajipange na kuwaeleza kuwa atakwenda kwenye kikao chao ambacho mrejesho wake atampa Makalla ambaye ni Mlezi wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Baadhi ya wananchi wakizungumza na mwandishi wa habari hii mara baada ya mkutano huo akiwamo Japhet Lema, mkazi wa Mchikichini, walisema Halmashauri ya Wilaya ya Ilala katika maeneo mbalimbali kumekuwa na kero hiyo ya utiririshaji majitaka.

"Kuna baadhi ya maeneo ambayo yameunganishwa na mfumo wa majitaka kuelekea baharini, mfumo huu iwe jua au mvua ukizidiwa utakuta chemba zake zinamwaga maji barabarani au katika makazi ya watu," alisema.

Sophia Mohamed, mkazi wa Kariakoo, alisema changamoto ya majitaka inatakiwa kushughulikiwa kwa haraka kwa sababu inaharibu hadhi ya Jiji la Dar es Salaam.

"Fikiria wageni wanaoingia kila siku Soko Kuu la Kimataifa Kariakoo, kila wanakokanyanga ni haja kubwa na sehemu nyingine unakuta kuna chemba imezidiwa inamwaga majitaka na pembeni kuna mgahawa au mamantilie.

"Wananchi inatukera sana kwa kuwa tunalipia huduma hii, lakini hali ni mbaya. Kwa kuwa serikali imebeba jukumu la kukusanya fedha zetu za majitaka kwa tulioungwa katika mfumo wa kuyapeleka baharini, wawajibike kuyakomesha," alisema.

Sophia alisema kama mfumo huo umezidiwa kulingana na idadi ya watu waliounganishwa awali ni vizuri ukafumuliwa upya na kuboreshwa zaidi ili maji yanapotoka kwenye makazi yaende moja kwa moja baharini na si kutiririka mitaani.

"Zipo baadhi ya nyumba ambazo ziliunganishwa katika mfumo huu karibu na chemba kubwa ambazo mfumo ukizidiwa maji yanarudi katika makazi ya watu, haya yote ni ya kuangaliwa na kuboreshwa," alishauri.



Mkuu wa Wilaya Kisarawe, mkoani Pwani, Petro Magoti (wa tatu kushoto), akizungumza na mjasiriamali wa bidhaa za chakula katika Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), juzi.
**PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# 16,000 wachaguliwa kujiunga vyuo vya afya

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) limesema jumla ya wanafunzi 16,646 wamechaguliwa kujiunga na vyuo 221 vinavyotoa programu mbalimbali za afya na sayansi shirikishi kwa mwaka wa masomo 2024/25

Mkurugenzi wa Udahili, Utahini na Utunuku, Marcelina Baitilwake, alisema juzi kuwa miongoni mwa waliochaguliwa, wanawake ni 8,821 na wanaume ni 7,825.

Alisema hayo ni matokeo ya uchaguzi wa awamu ya kwanza kwa walioomba kujiunga na programu za afya na sayansi shirikishi kwa mwaka wa masomo 2024/25.

Alisema jumla ya waombaji 24,629 waliwasilisha maombi yao kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (CAS) na waombaji 23,503 walikamilisha maombi yao kwa kuchagua vyuo/programu walizozipenda.

"Waombaji 21,661 walikuwa na sifa kwenye programu walizoomba na waombaji 1,842 hawakuwa na sifa kwenye programu walizoomba," alisema.

Alishauri waombaji wenye sifa ambao hawakuchaguliwa kutokana na ushindani katika programu na vyuo walivyoomba, waombe kujiunga katika programu na vyuo vyenye nafasi katika dirisha la awamu ya pili kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja.

Alisema dirisha la awamu ya pili lilifunguliwa rasmi jana na litakuwa wazi hadi tarehe 10 Agosti 2024, matokeo ya uchaguzi yatatolewa mwezi ujao.

Meneja wa Kitengo cha Utunuku, Twaha Twaha, alisema jumla ya vyuo 221 vinavyotoa kozi za afya vimeshiriki kwenye udahili huo kupitia mfumo wa pamoja.

Alisema vyuo hivyo vinatoa jumla ya kozi 13 ambazo zilizohusika kwenye udahili huo na kwamba ambao hawakuchaguliwa wamekosa vigezo mbalimbali vilivyohitajika.

"Mwombaji wa kozi yoyote kwenye chuo kabla ya kuomba anatakiwa ajiridhishe kama ana sifa zinazohitajika kwenye hiyo kozi na hizo sifa zipo kwenye mwongozo wa udahili wa wanafunzi student admission guide book na kipo kwenye tovuti yetu," alisema

Alielekeza wanafunzi wanaotaka kusomea kozi mbalimbali kutafuta mwongozo huo na kuangalia kama wana sifa badala ya kuomba moja kwa moja bila kuwa na taarifa kamili.

"Kwa kutumia mfumo wa udahili wa pamoja, tumeleta uwazi katika kufanya maombi kwani mwanafunzi anaona nafasi ziko kiasi gani na wanafunzi wangapi wameshaomba na baada ya kutoa majibu mwanafunzi anaona kwanini hakuchaguliwa.

"Anaona ushindani uliopo na nafasi zimejaa, hivyo tunatoa nafasi kwa awamu zinazofuata ili waweze kuomba kwenye vyuo vyenye nafasi na wakati wa kuomba mwanafunzi yeyote anapoingia katika mfumo kuomba tena, anaomba kwenye chuo kingine chenye nafasi na hawatoi fedha tena," alisema.

Aliongeza kuwa mfumo wa udahili wa pamoja umekuwa na manufaa makubwa kwa kuwa umekuwa ukipunguzia waombaji gharama za kuomba nafasi vyuoni.

"Mfumo huu unampunguzia gharama za kudahiliwa na gharama za kusafiri kutoka sehemu alipokwenda kwenye chuo kuomba udahili kwa sababu kuna vyuo ambavyo havina mifumo ya kumwezesha mwanafunzi kudahiliwa mtandaoni," alisema Twaha.

Alisema kupitia mfumo huo mwanafunzi popote alipokaa akiwa na kompyuta yake au simu ya mkononi anaweza akafanya maombi na kufuatilia hatua kwa hatua mwendendo wa mchakato wa udahili.

Alisema kabla ya kutoa matokeo hayo, NACTVET ilikutana na wakuu wa vyuo vyote vilivyohusika na udahili huo na kuwasilisha mada kuhusu namna mchakato mzima wa kuchagua wanafunzi ulivyofanyika.

"Kikao kiliamua kwamba matokeo yanaweza kutoka na kuna mambo ambayo tumekubaliana waombaji wazingatie na wenye vyuo wazingatie hayo na ushauri wetu NACTVET kwa wanaotaka kujiunga na kozi za afya wahakikishe wamefanya maombi kabla ya tarehe 28 mwezi Septemba," alisema.

Alisema baada ya hapo hakutakuwa na nafasi kwa mtu yeyote kujiunga na kozi za vyuo vya afya kwa sababu dirisha la kuomba nafasi hizo litakuwa limeshafungwa.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**






Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akimwonyesha Naibu wake, Khamis Hamza Khamis, ujumbe aliotumiwa na mwananchi kuhusu kurejea kwa mifuko ya plastiki, wakati akizungumza na menejimenti ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waomba huduma matibabu kibingwa kufika ngazi ya kata

**Gideon Mwakanosya,**
NAMTUMBO

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Baraka Ndelwa, ameishauri serikali kufikisha huduma za kibingwa za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo ngazi ya wilaya na kata ili kuokoa maisha ya watu ambao wengi ni wa kipato cha chini.

Dk. Ndelwa alitoa ushauri huo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kituo cha afya Lusewa, wilayani Namtumbo, kilichopo umbali wa kilometa 200 kutoka makao makuu ya wilaya.

Alisema ni kwa mara ya kwanza kutoa huduma za upimaji na uchunguzi wa magonjwa ya moyo kupitia taasisi hiyo kwa kufika katika vituo vya afya ngazi ya kata.

Alisema katika vituo hivyo wamebaini kuwapo kwa changamoto mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa baadhi ya vifaa muhimu vya upimaji wa magonjwa hayo.

"Mara nyingi tunafanya kazi hizi ngazi ya mkoa na katika kumbukumbu zangu hatujawahi kufanya kazi ngazi ya wilaya na kata. Mara nyingi tunaishia katika hospitali za rufani, hii ni bahati kubwa sana kwangu nimejifunza huku chini kupoje," alisema Dk. Ndelwa.

Aidha, tangu kuanza kwa mchakato huo wamefikia zaidi ya wagonjwa 258 waliofanyiwa vipimo vya magonjwa ya moyo.

Dk. Ndelwa alisema waliofanyiwa uchunguzi kwa kipimo cha ECHO ni 185, kipimo cha umeme wa moyo 89 na wagonjwa wanne wamepewa rufani ya kwenda JKCI Dar es Salaam kwa ajili ya vipimo na ikiwezekana kupatiwa matibabu zaidi.

Mtaalam huyo alishauri umuhimu wa wananchi kujenga tabia ya kwenda kuchunguza afya zao mara kwa mara kutokana na idadi kubwa ya watu wenye shinikizo la damu kutofahamu hali zao.

Mbunge wa Namtumbo, Vita Kawawa, aliwataka wananchi wa Kata ya Sasawala na maeneo mengine kujitokeza kwa wingi kwenda kupima afya zao, kwa kuwa ni bure na kufanyika kwa mara ya kwanza ngazi ya kata, likihusisha madaktari bingwa.

"Kiongozi anajivunia kuongoza wananchi wenye afya bora ili kuwasaidia kujiletea maendeleo zaidi katika maeneo wanayoishi na huku ukizingatia asilimia kubwa ya wananchi tunategemea kilimo," alisema Kawawa.

Athumani Haule, mkazi wa Kijiji cha Ligunga, alisema kituo cha Afya Lusewa kipo mbali na Hospitali ya Wilaya Namtumbo, ujio wa mabingwa hao umesaidia wananchi kupatiwa huduma na kujua matatizo yanayowasumbua kiafya.

Kaule aliiomba serikali kuweka utaratibu wa madaktari bingwa kufika mara kwa mara katika vituo vya afya nchini ili kusaidia kutoa huduma za kibingwa.

Pilly Said, mkazi wa Lusewa, alisema alifika katika kituo hicho kwa ajili ya matibabu kuambiwa ana changamoto katika moyo, lakini baada ya kukutana na mabingwa hao tatizo limeonesha linatokana na acid (tindikali) kwenye mfumo wa chakula.

Diwani Kata ya Lusewa, Said Zidadu, alisema huduma inayotolewa kituoni hapo ni muhimu kwa kuwa inasaidia watu kujua hali zao.

# TFRA yahakikishia wakulima upatikanaji wa mbolea nchini

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) imeahidi kuwa hadi mwishoni mwa mwaka huu itakuwa imefikia lengo la kuzalisha mbolea inayotosheleza mahitaji ya soko.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Antony Diallo, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, alipotembelea Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (Sabasaba) yanayoendelea.

Alisema lengo la Wizara ya Kilimo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030, Tanzania iwe na uwezo wa kuzalisha mbolea inayotosheleza mahitaji ya ndani na nyingine kuuzwa nje ya nchi.

"Si tu kusubiri mwaka 2030, kwa sasa tumeshaanza kuzalisha kiwango kikubwa cha mbolea na tunatarajia hadi mwisho wa mwaka huu, tutakuwa na uwezo wa kuzalisha kiwango chote cha mahitaji yetu," alisema Diallo.

Alisema upatikanaji mbolea nchini ni asilimia 80 hadi 90 na kwamba mahitaji ni tani 850,000 ambazo wanaweza kuzalisha nchini.

Mwenyekiti huyo alisema mamlaka hiyo ina jukumu la kuangalia maeneo ambayo yana matumizi ya mbolea na upatikanaji wake na namna inavyotumika ili kumrahisishia kazi mkulima kuipata.

Alisema kuna malighafi nyingi zinazalishwa nchini ambazo zinaweza kutumiwa kuzalisha mbolea kwa ajili ya kilimo, hivyo zinaweza kutumika badala ya kuagiza kiasi kikubwa cha mbolea kutoka nje ya nchi.

Diallo alisema maonesho hayo ni muhimu kwa kuwa watu kutoka mataifa mengine wanatembelea, hivyo ni fursa kwao kupata wanunuzi wa mbolea inayozalishwa Tanzania.

Aliwataka Watanzania kutembelea banda hilo ili kupata elimu kutoka TFRA na shughuli wanaofanya kwa maslahi ya sekta ya kilimo na taifa kwa ujumla.

# Katibu Mkuu asifu utolewaji elimu ya fedha kwa umma

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa amesifu utolewaji elimu ya fedha kwa umma unaolenga kukomboa wananchi kiuchumi, hivyo kuwasaidia kuondokana na umasikini.

Alitoa pongezi hizo juzi wakati akizindua msimu wa pili wa kipindi maalum cha televisheni cha elimu ya fedha kwa umma kinachoandaliwa na Benki ya CRDB,

Msigwa alisema elimu ya fedha itakayotolewa katika kipindi hicho itafungua Watanzania wengi juu ya fursa zilizopo katika taasisi za fedha zikiongozwa na Benki ya CRDB. Maarifa watakayoyapata pia yatawasaidia kujikomboa kiuchumi na kuliwezesha taifa kuyafikia malengo ya kuwa na uchumi jumuishi.

Katibu Mkuu huyo alisema kipindi hicho cha elimu ya fedha pia kinakwenda kusaidia kupambana na maadui wawili kati ya watatu waliotajwa na Mwalimu Julius Nyerere ambao ni ujinga na umasikini na hilo likifanyika, itakuwa rahisi kwa jamii kukabiliana na magonjwa.

"Ukishapambana na ujinga na umasikini ni rahisi kutafuta maarifa mengine yakiwamo ya kukabiliana na maradhi.

"Ninaawapongeza Benki ya CRDB kwa jitihada zenu za kuwaelimisha Watanzania. Kila mmoja akishiriki katika hili itakuwa rahisi kufanikisha malengo ya serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuboresha maisha ya Watanzania," alisema Msigwa.

Katibu Mkuu alisema kuwa fedha nyingi nchini zinazunguka katika sekta isiyo rasmi kwa kuwa wananchi wengi hawafahamu faida za matumizi ya huduma za benki.

Hivyo, wajasiriamali wengi wamekuwa wakijinyima fursa za kunufaika na mikopo pamoja na huduma nyingine za benki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema utoaji elimu hiyo ni sehemu ya utekelezaji Mpango wa Elimu ya Fedha (2021/22 - 2025/26) unaolenga kuongeza ufahamu na matumizi ya huduma za fedha kwa wananchi.

Mbali na hayo, Nsekela alibainisha kuwa hilo ni jukwaa muhimu la kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na akaunti za benki, kuwekeza na kutumia huduma za kifedha kwa usalama na ufanisi.

"Tukiwa benki kiongozi ya kizalendo tuna wajibu wa kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya fedha kwani kwa kufanya hivyo si tu tunasaidia kuchochea ujumuishi wa kifedha bali pia wa kiuchumi kwani elimu hii itasaidia watu kuchangamkia fursa za kiuchumi kutokana na maarifa waliyonayo ya huduma za fedha ambazo zinatolewa na benki yao ya CRDB," alisema Nsekela.

Aliongeza kuwa kupitia programu mbalimbali za elimu na uwezeshaji kwa jamii, Benki ya CRDB inaendelea kujitolea katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii kwa kuhakikisha huduma za kifedha zinawafikia watu wengi zaidi, hususan wale wa vijijini na maeneo yasiyo na huduma za benki.

Joseline Kamuhanda, Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Benki ya CRDB, alisema kuwa msimu wa kwanza wa elimu hiyo ulikuwa na mafanikio makubwa, hivyo wamefanya maboresho makubwa ili kurahisisha uelewa kwa wananchi.





# Naibu Waziri akunwa maandalizi maadhimisho ya mashujaa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga amesema ameridhishwa na maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa inayotarajiwa kufanyika Julai 25, mwaka huu jijini hapa.

Ummy alisema hayo baada ya kufanya ukaguzi na kuridhishwa na maendeleo ya maandalizi hayo yanayoendelea jijini hapa kwa kuwa yanaendelea vizuri, ambayo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Alisema maadhimisho hayo yatashirikisha gwaride la vikosi vya majeshi ya ulinzi na usalama vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Uhamiaji.

Awali akitoa maelezo kuhusu maandalizi hayo, Mkurugenzi wa Kitengo cha Maadhimisho na Sherehe za Taifa Ofisi ya Waziri Mkuu, Batholomeo Jungu, alisema yatatanguliwa na uwashaji Mwenge Julai 24, mwaka huu usiku, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

# Migogoro mgawanyo mirathi, ardhi yaongezeka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Sera na Mipango Wizara ya Katiba na Sheria, Mbaraka Stambuli amesema tabia ya baadhi ya watu kutokuwa na utaratibu wa kuandika wosia wa mali wakiwa hai ni chanzo cha ongezeko la migogoro kwa familia kwenye mgawanyo wa mirathi nchini.

Sitambuli alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao kati ya menejimenti ya wizara hiyo na kamati ya taifa ya ushauri kuhusu utekelezaji wa programu ya kizazi chenye usawa.

Alisema kupitia kampeni ya msaada wa kisheria inayotekelezwa na wizara hiyo inayojulikana kama Mama Samia Legal Aid katika mikoa saba, wametoa huduma za migogoro, iliyoongoza ni mirathi na ardhi.

Alisema kutokana na hali hiyo, wametoa elimu kwa wananchi kujenga tabia ya kuandika mirathi wakiwa hai ili kuondoa usumbufu kwa familia zao kwa kukumbana na migogoro isiyoisha na kusambaratika.

"Kuandika mirathi kutasaidia ndugu, watoto pamoja na jamaa wa karibu wenye maslahi na mali hizo kuondokana na migogoro na usumbufu unaweza kujitokeza baada ya mmiliki kufariki dunia," alisema Stambuli

Akizungumzia uhusu migogoro ya ardhi, alisema wamebaini tatizo lipo kwenye elimu na kusababisha wanawake wengi kupoteza haki ya kumiliki.

"Kupitia kampeni hii ya msaada wa kisheria ya Mama Samia tunaendelea kutoa msaada wa kisheria kwa wanawake, moja ya changamoto ambayo tumeibaini ni ukosefu wa elimu, wanawake wengi hawajamiliki ardhi kisheria, hawana hati miliki za kimila au kisheria.

"Tunawashauri kutumia fursa ya umiliki wa mke na mume katika hati moja ili kuondokana na changamoto ambazo wanaweza kukumbana nazo za kukosa haki ya kumiliki ardhi,"alisema Stambuli.

Akizungumzia kuhusu kampeni hiyo, alisema kutokana na mahitaji makubwa ya wananchi kwenye usaidizi wa kisheria, wameongeza bajeti ili kufika mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema katika mwaka huu wa fedha wa 2024/25, bajeti ya kampeni hiyo imeongezeka mara tatu kutoka Sh. bilioni mbili hadi sita ili kusaidia kumfikia kila mwanachi na kutoa usaidizi wa kisheria.

Waziri wa Maliasili na Utalii na Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Ushauri kuhusu utekelezaji wa programu ya kizazi chenye usawa, Angellah Kairuki, aliiagiza wizara hiyo kushirikiana na kamati yake kutatua kero zinazowakabili wanawake.

"Mnapotekeleza kampeni hii ya msaada wa kisheria pia kamati hii ipate ripoti ili kuona ni namna gani tunaweza kufanya kazi kwa pamoja na kufikia azma ya Rais wetu ya kuwa na kizazi chenye usawa bila kumwacha mtu nyuma," alisema.

Alisisitiza Wizara ya Katiba na Sheria kutupia jicho kwa makundi maalum na maeneo ya vizuizi, ikiwemo mahabusu na magereza ili kuwasaidia wasiokuwa na uwezo wa kupata msaada wa sheria.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikagua maendeleo ya ujenzi wa Mnara wa Mashujaa katika mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma jana, ikiwa ni maandalizi ya Siku ya Mashujaa itakayofanyika mkoani humo Julai 25 mwaka huu. **PICHA: OWM**

# 'Msiwachague viongozi ambao ni wala rushwa'

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANANCHI wametakiwa kuchagua viongozi wenye sera na mipango madhubuti kwa ajili ya kuleta maendeleo nchini.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024, Godfrey Mnzava, akizungumza juzi kwenye Viwanja vya Bombadia Manispaa ya Singida mkoani hapa wakati wa mkesha aliwaonya wananchi wasithubutu kuchagua wagombea watoa rushwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji baadaye mwaka kuu kwa kuwa watachelewesha maendeleo yao na kujinufaisha kwa maslahi binafsi.

"Msichague viongozi wanaotoa rushwa watawarudisha nyuma kwa sababu hawataleta maendeleo bali watajiangalia wao tu, " alisema.

Akiwa wilayani Mkalama, Mnzava aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika nchini Novemba mwaka huu.

"Uchaguzi upo tayari mlangoni, tujitokeze kwa wingi kushiriki ku chagua viongozi wetu, tukio la kupiga kura halitachukua muda mrefu, twendeni tukapige kura. Pia tulinde amani na umoja wakati wa uchaguzi," alisema.

Akizungumzia mabadiliko ya tabia nchini, Mnzava, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kukata miti ovyo na kujikita katika upandaji miti ili kuepukana na madhara yanayotokana na uharibifu wa mazingira.

"Tuchukue wajibu wa kulinda mazingira yetu, nimepita Shule ya Mkalama One nimeona kazi nzuri, nimeona mmeanzisha mradi wa mazingira. Tukifanya hivi tutakuwa vinara katika mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira," alisema.

Awali akizungumzia miradi iliyopitiwa na mwenge huo, Mnzava ameipongeza Mkalama kwa usimamizi mzuri wa fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mwenge huo kwa Mkalama, umezindua mradi mmoja na kuweka jiwe la msingi miradi miwili, miradi hiyo mitatu, ina tham an i ya Shilingi 2,067,623,126.

Kauli ya mbio hizo kwa mwaka huu "Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.





## Mradi kunufaisha vijiji Chakwa, Nungwi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa vijiji vya Chwaka na Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja wametakiwa kushiriki katika mradi wa kushirikisha jamii kuimarisha sekta ya utalii na kuleta mageuzi ya kiuchumi katika maeneo hayo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Aboud Suleiman Jumbe wakati akizungumza na wakazi hao kuhusu utekelezaji wa mradi huo ambao umelenga kuleta mageuzi kwao ili kufaidika na fursa za utalii katika maeneo ya ukanda wa fukwe.

Jumbe, alisema sekta hiyo dhana yake ni kuanzisha ujenzi wa hoteli za kitalii, kazi za kutembeza watalii na wananchi kuuza bidhaa za kilimo na uvuvi.

Alisema mradi huo umelenga kuwashirikisha wananchi ikiwemo wavuvi wa ukanda wa bahari katika vijiji kwa kuuza samaki na mazao ya baharini.

Alisema katika Kijiji cha Nungwi chenye zaidi ya hoteli za kitalii 78, wavuvi wana fursa ya kuvua samaki, kuuza katika hoteli hizo na kujipatia fedha.

"Tunataka kuona wavuvi wetu wanazilisha hoteli zote ziliopo ukanda wa Nungwi kwa kuvua samaki katika dhana kubwa ya kunufaika na utalii," alisema.

Baadhi ya wakazi hao, walifurahishwa na mradi huo kwa kuwahakikishia kupata soko la kuuza bidhaa zao bila ya matatizo.

Mvuvi, Ali Issa Juma, alisema wanavua samaki wakubwa, lakini hawana uhakika wa kupata soko la kuwauza.

Alisema mradi huo utawaunganisha moja kwa moja na wamiliki wa hoteli hizo na kupata soko la uhakika na kipato kwa familia zao.

Mwekezaji wa hoteli, Joel Clement Hart, alisema wapo tayari kufanya kazi na wavuvi na wakulima ili wanufaike na mnyororo wa thamani katika sekta ya utalii nchini.

# Dk. Mwinyi asifu sheria kwa watoa taarifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi amesema sheria ya kumlinda mtoa taarifa itasaidia kuimarisha ulinzi, kuwatia motisha na kulipa fidia kwa watoa taarifa, mashahidi na kuwaongezea imani na usalama wa maisha yao.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika Maadhimisho ya Siku ya Mapambano dhidi ya Rushwa Afrika yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya Nyamanzi Unguja visiwani hapa.

Alisema Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) inaendelea kutekeleza majukumu yake chini ya sheria nambari 5 ya mwaka 2023, sheria ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar baada ya kufutwa kwa sheria namba 1 ya mwaka 2012.

"Kufutwa kwa sheria hii kumetokea baada ya kubaini kuna umuhimu wa kuifanyia marekebisho ambayo yataenda sambamba na mabadiliko na kasi ya usimamizi wa mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi nchini, " alisema Dk. Mwinyi.

Alisema miongoni mwa marekebisho yaliyofanyika ni pamoja na kifungu cha 98 cha sheria ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar namba 5 ya 2023 ambacho kinatoa mwongozo wa kumlinda mtoa taarifa na shahidi na kuwepo usiri wa kutojulikana kwa watu hao kutokana na ushirikiano wanaoutoa kwa mamlaka.

Alisema pamoja na hayo, zipo sheria zinazosimamiwa na taasisi ambazo zinatoa utaratibu wa namna ya kuwalinda watoa taarifa dhidi ya changamoto za kiusalama pindi wanapotekeleza jukumu hilo.

Alisema sheria hizo ni za utumishi wa umma ya mwaka 2011, sheria ya ukaguzi wa umma namba saba ya mwaka 2023, sheria ya mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya Zanzibar namba 8 ya mwaka 2021 na sheria ya ushahidi namba 9 ya mwaka 2016.

"Ukweli ni kuwa rushwa hudhoofisha mifumo ya kitaasisi na kuathiri mipango ya maendeleo ya kiuchumi ambayo makosa yake ni miongoni mwa makosa yanayovuka mipaka".alisema

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, lazima kutekeleza mikatabaya kupambana na rushwa ili kufikia malengo ya kimataifa ikiwemo kupeana misaada ya kisheria na ushirikiano wa kitaalamu ili kuongeza ufanisi wa kuchunguza na kurudisha mali zinazopatikana kwa njia za rushwa na makosa mengine ya uhalifu yanayovuka mipaka ya nchi.

Alisema jitihada kubwa zinafanyika Zanzibar na Tanzania Bara kupitia ZAECA na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

" Taasisi hizi zinafanya kazi kubwa ya kuelimisha jamii kudhibiti rushwa na uhujumu uchumi ili kuweza kupata matokeo chanya katika jamii," alisema.

Alisema katika kipindi cha Julai mwaka 2022 hadi Mei 2024 ZAECA imefanya ufuatiliaji wa fedha za miradi 115 na kutolewa ushauri.

Alisema katika kipindi hicho, ZAECA imechunguza na kukamilisha majalada 86 na kuyawasilisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na kwamba kwa ushirikiano wao wamepeleka majalada 29 mahakamani.

Naibu Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhwani Kikwete, alisema wizara hiyo kupitia TAKUKURU imekuwa na mikakati ya kupambana na rushwa nchini na kuwasisitiza watumishi wa umma na jamii kujiepusha na matumizi na vitendo hivyo kwa kuwa vinadhorotesha ustawi wa uchumi wa nchi.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA, Ali Abdallah Ali, alisema katika kipindi cha Julai mwaka 2022 hadi Mei mwaka huu, ZAECA imeokoa Sh. Bilioni 7.9 kwa kudhibiti ukwapajii, ubadhirifu wa mali, mapato na matumizi mabaya ya ofisi za Serikali.

Ali, alisema katika kipindi hicho, imefuatilia fedha za miradi ya maendeleo 115 kuanzia hatua ya awali hadi kukamilika na kutoa ushauri.




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kulia), akipokea Mwenge wa Uhuru Mwaka 2024 kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, katika Kijiji cha Gehandu, wilayani Hanang jana, ambapo unatarajiwa kutembelea miradi 57 yenye thamani ya Sh. bilioni 149.5. **PICHA: MARY MARGWE**

# ZHSF yaboresha huduma kwa wanachama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar (ZHSF), Yasin Juma Ameir amesema utaratibu wa rufaa walioweka, utatoa fursa kwa wanachama wao kupatiwa huduma za matibabu kwa wakati mmoja.

Juma alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mafunzo ya kuwajengea uelewa kuhusu upatikanaji wa huduma za afya bora za mfuko huo nje ya Zanzibar.

Alisema mfuko umefanya baadhi ya mabadiliko ya rufaa kwa mwanachama wake kuanzia ngazi ya zahanati mpaka wilaya bila ya rufaa.

Alisema wamefanya hivyo ili kutoa nafasi kwa madaktari bingwa kuhudumia matatizo yanayokwaza wagonjwa.

"Haiwezekani sote tukakusanyika pamoja na mwenye maradhi tofauti katika sehemu moja na huu utaratibu wa rufaa maana yake kila mmoja atatawanyika sehemu tofauti," alisema.

Hata hivyo, alisema kukusanyika pamoja pia kuna athari ya watu kutumia muda mwingi kuweza kuonana na daktari na wakati mwingine kukosa fursa hiyo. "Sote tunajua Wazanzibar wote hawa milioni 18 uwakusanye katika hospitali chache, kuna mtu ana mafua, muwasho, au kuumwa kichwa, aliyevunjika mguu na anayetaka kusafishwa figo, sote tupo katika hospitali moja tunamsubiri daktari bingwa atuhudimie na hapo utakuta kuna foleni," alisema.

Alisema kuweka rufaa kumekuja baada ya mfuko huo kufanya tathmini ili kuhudumia wanachama wake kwa ufanisi zaidi.

"Tunajua matibabu ni gharama na sisi tunalipa madaktari, kila mmoja ana gharama zake, sasa mtu atakuwa radhi akamlipe daktari bingwa kwa mgonjwa ambaye amekwenda kwa maradhi ya mafua au kichwa na muwasho," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Udhibiti, Ubora wa Huduma za Afya (ZHSF), Dk. Habiba Sultani Mbwana, alisema pamoja na kuwa kuna rufaa, haizuii hospitali kupokea wagonjwa wa rufaa baada ya kufikishwa kwa dharura.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa ni wananchi wengi kuugua magonjwa sugu kwa kutumia dawa zisizo sahihi kwa kuwenda kwenye vituo vya afya.

Aliitaka jamii kufuata utaratibu wa mfuko wa kufuata matibabu ngazi kwa ngazi.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usajili na Usimamizi wa Wanachama wa mfuko huo, Ali Idrisa Abeid, alisema malengo ya mfuko ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wakazi wote wa Zanzibar na kuwepo rasilimali fedha za kutosha za endelevu kwa ajili ya kugharamia huduma za afya.



BRITNEY HATAKI MCHEZO Uk.14



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

# INGEKUWAJE UNGEONDOKA?



MWANASOKA wa Yanga, Aziz Ki ambaye usajili wake umekuwa gumzo, amezidi kuwashika wapenda burudani baada ya kuonyesha kudata kimahaba na mwigizaji na mwanamitindo Hamisa Mobetto.

Mobetto ambaye amehusishwa kutoka kimapenzi na mwanasoka huyo, amekuwa akitupia picha na video katika ukurasa wake wa Instagram, akiwa kwenye mapozi tofauti na mwanasoka huyo.

Kile ambacho kinaonekana sasa wawili hao wamegandana kama njiwa, wameandika jumbe ambazo zinaashiria suala la Ki kuendelea kubaki Yanga limewapa ahueni kwao.

Katika chapisho moja la picha inamuonyesha Mobetto na Ki wakicheza mpira pamoja, mrembo huo aliandika ujumbe unaosema “Sasa ungeondoka ingekuaje?”

Kisha Ki alimjibu haraka “Ningeenda wapi wakati wewe uko hapa”.

Baadhi ya watu walioshiriki chapisho hilo walitoa maoni tofauti, huku idadi kubwa wakieleza kufurahishwa kwao kwa penzi hilo zito wanaloonyesha mastaa hao.

Walieleza pamoja na wawili hao kufurahia mahaba, lakini washabiki zao wanapata raha kutokana na kile wanachokifanya wakiwa nje ya kazi zao.

BASI SAWA

## Msikieni Omondi anachosema



MSANII wa uchekeshaji kutoka Kenya, ambaye kwa sasa amekuwa mwanaharakati, Eric Omondi, ameibua mjadala baada ya kueleza kabla ya Rais William Ruto hajavunja baraza la mawaziri, tayari alikuwa na taarifa hiyo.

Akizungumza kwenye runinga ya Citizen, amesema alipata taarifa hiyo kwa mtu ambaye hakumtaja jina kwamba kuna uhakika wa kuvunjwa kwa baraza la mawaziri usiku wa Alhamisi.

"Kumbuka Jumanne nilikuwa nimemuomba Rais Ruto kulivunja baraza lake la mawaziri kufikia Alhamisi, mimi nilijua kufikia Jumatano usiku wakati Moses Kuria alikuwa anaondoka katika studio hizi, kwamba Ruto amefuta mawaziri wote," amesema.

## Idris ana jambo lake



MSANII wa filamu nchini Idris Sultan, amesema Watanzania hawana muda wa kusubiri kuona matunda kutokana na safari yao ya Korea Kusini.

Sultani ameandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amewabeba sana wasanii wa filamu, kilichobaki kutimiza deni wanalodaiwa na wananchi.

"Bado kuna deni ambalo wasanii wenzangu tunadaiwa na wananchi na halihitaji kusubiri. Deni la kazi bora na za maana lilipwe tena kwa haraka. Ni haki yao ya wazi wazi. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameshatubeba parefu sasa kujiongeza nayo isiwe ya kusukumwa," ameandika Sultan.



## Kitopu cha Wema gumzo

MWIGIZAJI maarufu wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, amejikuta akiwapa taharuki mashabiki zake baada ya kuonekana akiwa na vazi ambalo linaonyesha sehemu kubwa ya tumbo lake.

Wema ambaye amejikusanyia Milioni 11.5 ya wafuasi katika ukurasa wake wa Instagram, aliweka video fupi kwenye ukurasa wake akionekana amevaa fulana fupi ya mistari myeupe na bluu, huku sehemu ya tumbo lake likiwa wazi.

Baadhi ya watu walioshiriki video hiyo walionekana kuwa na maoni tofauti, huku wengine wakidai msanii huyo kuna kitu anachoashiria na pengine inawezekana anatarajia kuwa mama.





## Harmonize hana baya

MWANAMUZIKI mkali wa Bongo Fleva, Harmonize, amesema amekuwa akimuheshimu sana mkongwe Ali Kiba, kiasi ambacho kazi yake ya kwanza ilitokana na msukumo wake.

Amesema kwamba kile anachoamini katika mafanikio ya muziki kuna mikono ya watu wengi na kwamba hawezi kubagua msanii ambaye anataka kufanya naye kazi.

"Msanii yeyote mimi sina noma naye, niko hivyo kwa sababu naamini kila mwanamuziki ana mchango wake ambao umenifanya mimi nikawa hapa," amesema Harmonize.

## Wasanii Bongo walioishi Marekani

**Na Adam Fungamwango**

KAMBI ni popote. Huo ni msemo wa watoto wa mjini, wakiwa na maana kuwa binadamu huwezo kuishi popote pale amb apo wanaona ana uwezo wa kuendesha maisha yake bila matatizo.

Katika kutafuta maisha haijalishi umezaliwa wapi na unakwenda kuishi, au kutafutia sehemu gani.

Ndiyo maana unaweza kuona mtu anaweza kutoka Dar es Salaam, sehemu inayoonekana ina viwanda na ajira nyingi, au Dodoma, lakini akaenda kuishi Lindi au Manyara.

Anaweza kutoka Tanzania na kwenda kuendesha maisha yake Afrika Kusini. Hii yote ni kuhangaika kusaka maisha.

Wapo wengi, wakiwa wametawanyika nchini mbalimbali za Ulaya na mabara mengine lakini leo tutawaangalia watano, ambao wameamua kuishi nchini Marekani.

Hata hivyo, taarifa zinasema wengine wao hawapo huko kwa kazi zao walizokuwa wakifanya hapa nchini, bali wanafanya shughuli zingine wakiwa wameoa au kuolewa na raia wa huko.

**5# Mabeste**

Ni msanii ambaye miaka alitamba sana miaka ya nyuma na kutoka ngoma mbalimbali zilizowachengua mashabiki kama, 'Sirudii Tena', aliomshirikisha Jux, 'Dole', 'Nashauri' alioimba na Peter Msechu na nyingine nyingi.

Itakumbukwa pia kuwa miaka minne iliyopita alivuma kwenye kusara za magazeti na mitandao ya kijamii kutokana na mgogoro wake na aliyekuwa mkewe, Lissa ambaye baadaye ilivunjika.

Kwa sasa anaishini nchini Marekani, na ana familia, ingawa inaonekana yeye hajaachana kabisa na muziki, kwani miezi tisa iliyopita alitoa ngoma moja, inayoitwa, 'Bao.'

**4. Vanessa Mdee**

Mwingine ni msanii maarufu wa kike wa bongo fleva, Vanessa Mdee, naye kitambo sasa yupo Marekani.

Alirejea hapa nchini mara moja kusalimia ndugu na jamaa, akiwa tayari na familia yake, akionekana kuwa na watoto wawili.

Anakumbukwa kwa ngoma zake kali alizozifanya miaka kadhaa nyuma kama, 'Nobody But Me', 'Never Ever', 'Bambino', 'Juu', 'Kisela' na nyingine nyingi.

**3 # Mzee Magali**

Jina lake kamili ni Charles Magali, moja ya wasanii waigizaji wa filamu mbalimbali nchini.

Huwa anaigiza kama mzazi mwenye pesa, wakati mwingine kubwa la maadui, na zingine zinazofanana na hizo.

Baadhi filamu alizocheza ni kama 'Nje la Lengo', 'Kutakapokucha', 'Sekunde Chache', 'The Stolen Will' na nyinginezo.

Baadhi walikuwa wanajiuliza ni kwa nini haonekani kwenye tamthilia na filamu zinazoonyeshwa kwa wingi miaka ya sasa kwenye vituo mbalimbali vya televisheni.

Sababu ni kwamba hivi sasa anaishi nchini Marekani, hivyo imekuwa ngumu kufanya kama mashabiki wake wanavyotamani.

**2# Izzo Bizness**

Ni msanii wa muziki wa kufokafoka. Alitamba sana ni ngoma zake kama 'Kidawa', 'Tumeoana', na zingine nyingi.

Kwa sasa yupo nchini Marekani na anaonekana amekuwa na familia huko.

**1# Diana Kimaro**

Nadhani mashabiki wa filamu wa zamani wanamkumbuka mwigizaji mmoja wa kike machachari, Diana Kimaro. Kwa muda mfupi tu baada ya kushirikishwa kwenye filamu ya Elizabeth Michael 'Lulu', akaondokea kuwa maarufu na kupata fursa ya kucheza nyingine kali kama 'Confusion', 'Danija' na nyingine nyingi.

Huyu dada kwa sasa anaishi nchini Marekani ambako tayari ametengeneza familia yake huko.



DIANA



## Simulizi: Kaniki nyeusi hata ikitakata

**Na Adam Fungamwango**

KUNA mtu anaweza kufanya jambo ambalo linaweza kuonekana kuwa ni baya kwenye macho ya watu, lakini kumbe lengo lake likawa zuri tu.

Hii inatufundisha binadamu kuwa na subira kwa kile ambacho mtu mwingine anakifanya.

Filamu ya 'Simulizi' inatufundisha hivyo. Pia kuna upande mwingine inatufundisha tusiwe na roho mbaya. Kumfanyia roho mbaya ili ufanikishe jambo lako ambalo unaona litakupa faraja ni dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu.

Imechezwa na wasanii Nasra Juma, Aldin Hilal, Mariam Bahati, Mwanansanda Radoda, Sofia Hamisi na wengineo.

Inaanza kuonyesha kuwa Asia na Ally ni mtu na mkewe na wanapendana sana. Hata hivyo, mama yake Ally hamtaki Asia. Ni kwa sababu hazai. Miaka kadhaa imepita sasa bila hata mkwewe kuhitaji ndimu.

Katika pitapita zake, anamkuta msichana mmoja anaitwa Sofia. Huyu ni mchumba wa Hilal. Lakini mama huyo anataka aachane na Hilal ili aolewe na kijana wake Ally.

Wakati Asia akipata manyanyaso kutoka kwa mama mkwe, kuna kijana mmoja anaitwa Ligo. Huyu halali wala hali kwa kumpenda Asia. Kila akikutana na Asia anamweleza kuhusu jambo hilo. Asia anamwambia ameshachelewa kwa sababu tayari ameshaolewa. Ligo anabaki anaugulia moyoni.

Mama Ally kila siku anamwambia kijana wake aachane na Asia, lakini Ally anakataa kwa sababu anampenda. Kuna siku mama Ally alimshuhudia mkwewe akiwa amesimamishwa na Ligo, akiendelea na 'saundi' zake. Asia anazidi kumuelezea msimamo wake. Ni wakati ambao mama anakwenda kumwita kijana wake ili ashuhudie. Ally wivu unamshika. Anachoamua ni kumpa talaka mkewe. Mama anafurahi na kwenda kumueleza Sofia kuwa tayari Ally ameshaachana na Asia. Sofia anampasha kuwa hawezi kuolewa na Ally kwa sababu ana mchumba wake anaitwa Hilal.

Mama Ally anachukia. Kwa sababu ni mchawi, anampoteza Sofia na kumfanya msukule.

Asia sasa anakuwa huru kuishi na Ligo, na baada ya muda anakuwa mjamzito. Hilo linazidi kumkera mama Ally. Anamroga Asia na kumfanya mwendawazimu.

Zaina, dada yake Hilal, anapewa nguvu zisizo za kawaida na bibi mmoja wa kijiji cha jirani, kutokana na ukarimu wake. Ndiye anayekuja kuwaokoa Asia, kumrudishia akili za kawaida na kumponya Sofia aliyefanywa msukule. Asia akaendelea kuishi na Ligo, Sofia na Hilal. Mama Ally na uchawi wake akaungua moto kimiujiza.



# Britney hataki mchezo

STAA wa muziki wa Pop, Britney Spears ameamua kumuacha mpenzi wake Paul Soliz, baada ya kugundua kumweka mtu wa siri ili kumchunguza.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Britney na Paul walitengana wiki 3 zilizopita, licha ya kuwa walipendana lakini alikasirishwa kitendo cha kuwepo mtu huyo ambaye alikuwa akifanya kazi maalum ili kujipatia pesa.

Katika chapisho la Britney katika ukurasa wake wa Instagram, alimshutumu Paul kwa kuruhusu paparazi kupata picha yao wakiwa ndani ya gari lake wakati wakiwa kwenye mahaba kwa nia ya kujitajirisha.



## Kuti mke anataka matunzo

MWANAMUZIKI wa Afrobeat, Seun Kuti amefichua kwamba changamoto anayopata katika ndoa yake ni kumpa mkewe pesa za matumizi kila siku.

Akizungumza hivi karibuni, Kuti amesema katika ndoa yake na mkewe Yetunde, imetawaliwa na maisha ya furaha, lakini linapokuja suala la kutoa pesa limekuwa gumu kutokana na mke wake kutaka kiasi kikubwa.


"Posho yake ni kubwa sana, unatoa mara saba kila mwezi. Sifanyi mzaha; posho yake ni kubwa sana na anakulaghai kwa lugha laini, ni changamoto kwa sababu natakiwa kufanya kazi," amesema Kuti.

## Toyin umelitafuta/ sasa ulimalize

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Toyin Abraham, anakabiliwa na shinikizo kutoka kwa watu mbalimbali kutokana na kudaiwa kusababisha mama wa mfuasi wake katika mtandao wa kijamii kukamatwa na polisi.

Wakati wa kipindi chake cha moja kwa moja kupitia ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo alikanusha madai hayo, akisema kuwa yeye aliwasilisha ombi dhidi ya wanyanyasaji wa mtandaoni baada ya kukashifiwa mtandaoni.

Toyin alilalamika kuonewa mtandaoni kwa sababu aliimuunga mkono Rais Bola Tinubu wakati wa uchaguzi mkuu uliopita.





## Kris Jenner kufanyiwa upasuaji

MAMA mzazi wa Kim Kardashian, Kris Jenner, amefichua kuwa ana uvimbe katika mirija yake ya uzazi na anatakiwa kufanyiwa upasuaji ili kuokoa maisha yake.

Kupitia kipindi kinachoonyesha maisha ya familia Kardashian, kilichorushwa Jumatano, Jenner amesema ameanza kukutana na daktari ambaye angemfanyia upasuaji.

Amewaambia watoto wake kuwa ana wasiwasi kuhusu ukuaji wa uvimbe huo na anaona ni bora kuondoa.

## Hatimaye Celine Dion kutumbuiza

MWANAMUZIKI mkongwe ambaye anapambana na maradhi, Celine Dion, hatimaye ataonekana hadharani akitumbuiza katika ufunguzi wa michezo ya Olimpiki itakayofanyika mwaka huu nchini Ufaransa.

Celine ambaye ana 66 za Grammy. Anapambana na ugonjwa usio wa kawaida wa misuli na kumfanya kuahirisha matamasha yake ya muziki akihangaikia matibabu.

Maonyesho ya muziki kutoka kwa watu mashuhuri sio jambo geni kwenye michezo ya Olimpiki, kwani utamaduni huo ulianza katika karne ya 20, na maonyesho ya kwanza yalianzia 1896 huko Athene, Ugiriki.

Kulingana na mtandao wa Guardian, Celine pamoja na wasanii wengine Dua Lipa, na Aya Nakamura watapamba jukwaa katika ufunguzi huo.





# Wachomwa moto kwa wizi wa simu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANANCHI wanaosadikiwa kuwa na hasira kali wa Mtaa wa Shivazi Kata ya Kaloleni jijini hapa, wamewachoma moto vijana wawili waliopakizana kwenye pikipiki baada ya kudaiwa kupora simu.

Akizungumza jana eneo la tukio Kaloleni, Wille Lema alisema baada ya vijana hao kupora simu ya kijana mmoja mtembea kwa miguu, wananchi hao waliwazingira na kuwaamuru warudishe simu hiyo kwa mmliki wake, walikataa.

"Tulipowabana warudishe walikataa kuwa wao sio wezi wakati tumewaona, kilichofuata watu wenye hasira wakaanza kuwapiga na kuwachoma moto na pikipiki yao," alisema

Alisema baada ya kuwachoma moto , askari wa Jeshi Polisi walifika kwenye eneo la tukio na kuwachukua vijana hao wakiwa wamejeruhiwa vibaya na pikipiki.

Shuhuda mwingine, Lilian Shayo alidai kuwa:

"Shida vijana siku hizi hawataki kufanya kazi wanataka kupata pesa za haraka haraka na matokeo yake ni haya, watu wamechoka na sasa wanachukua sheria mkononi." Aliwaomba wazazi kuwakanya vijana wao waache wizi wa mali za watu na kufanya kazi halali za kuwaingizia kipato.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Arusha, Justine Masejo hakupatikana kuzungumzia tukio hilo kwa kile kilichoelezwa kuwa alikuwa kwenye kikao na Mkuu wa Mkoa Paul Makonda.

# Makonda asimulia Jenerali Mabeyo alivyomuokoa sakata la makontena

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amesimulia namna alivyookolewa na aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Venance Mabeyo katika sakata la makontena ya vifaa vya ofisi za walimu wa Dar es Salaam kwa kuwa kuna watu walitaka kumchomekea matrekta na magari kwenye makontena hayo.

Makonda aliyasema hayo jana jijini hapa alipokutana na wadau wa mashirika na asasi za kiraia kujadiliana masuala mbalimbali, ikiwemo changamoto zinazowakabili.

Alisema pona yake ni Jenerali Mabeyo kuzuia makontena yasifunguliwe na ulinzi kuendelea kuimarika, la sivyo matrekta na magari yangewekwa katika makontena hayo ili ionekane hakuleta thamani bali ni magari yake.

"Kipindi kile namshukuru Mungu baada ya kugundua taarifa walizozipeleka kwa Rais John Magufuli ni tofauti na uhalisia usiku walitaka kwenda kufungua yale makontena waweke matrekta na magari ili nionekane nilikuwa nadanganya naleta vifaa vya walimu kumbe naleta vya kwangu," alisema.

Makonda, alisema kulikuwa na wanajeshi wanalinda makinikia ambao wapo chini ya Jenerali Mabeyo walivyowakuta wakaogopa.

"Mabeyo akaweka ngumu hakuna kufunguliwa makontena. Hiyo ilikuwa salama yangu hizi nia njema zina nyakati ngumu sana ... halafu huku nimeshatangazwa huyo mkwepa kodi, fisadi anataka kujitafutia mali,"alisema Makonda na kuongeza kuwa:

"Mimi ni mmoja wa wahanga wa haya mambo ya ufadhili Dar es Salaam nilifanya ile kazi ya ujenzi wa ofisi za nyumba za walimu kwa nguvu kubwa nikaomba wadau wa malori, watu wa vituo vya mafuta wakatoa mafuta, Magereza wakatoa watu, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) wakatoa vifaa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wakatupatia askari tukaanza kujenga ofisi za walimu."

Alisema wakapatikana watu wengine wema kutoka nchini Marekani walijitolea kontena 20 zilizokuwa na thamani.

"Zikaingia siasa pale zilikuwa siasa kali kweli kweli, kumbe kuna jamaa wanasema huyu akiendelea hivi na walimu wakimpenda atatusumbua mbele ya safari,"alisema Makonda.

Alisema wakati anapambana kuleta maendeleo kwa walimu wakae katika ofisi nzuri na kuheshimika kumbe kuna baadhi wanawaza tofauti.

"Nilipigwa fitina ambayo sijawahi kuiona duniani ikafika mahali nikasema sasa watajua Mungu yupo ama hayupo. Nikasema hata wakitafuta wateja hawatauza na atakayenunua atalaaniwa yeye na kizazi chake," alisema.

Makonda, alisema anakumbuka wakati ule bosi wake alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Seleman Jafo, aliandika barua na kuelezea msaada huo, ilishindikana na kuendelea kushikiliwa kooni.

"Njemba zimekaa vikao vya usiku wakati huo sikuwa najua yale maombi ya kusambaratisha vikao vya sirini kwa sasa nimeshayajua sasa ninawakung'uta na vikao vyao vya usiku wanavyovifanya," alisema.

Alisema anaelewa asasi za kiraia zinapata changamoto sio kwa sababu wanaleta vitu kwa ajili ya kuuza bali wengine ni kuoneana wivu.

Alisema kulikuwa na upungufu wa vifaa kwa ofisi za walimu zaidi ya 400 wanakaa chini ya miti, aliomba wadau, hajatumia fedha ya serikali, mtu mmoja anaungana na mwenzake kuharibu.

"Umoja wa waovu huwa haudumu, wanasambaratika tukikutana wananiambia mheshimiwa vipi nawambia kwa neema nimerudi wewe je? Utasika kwa kweli unatutia moyo sana, tukikutazama," alisema Makonda.

Alisema kuna mmoja alikutana naye kwenye kahawa akamueleza wao ni wale wa Magufuli wanaonewa. "Nikamuambia acha uongo haukuwa wa Magufuli acha unafiki wewe yaani mtu anataka kutengeneza chuki kama una sifa zako utafanya kazi kama hauna sifa hautafanya kazi," alisema.

Makonda amezitaka asasi za kiraia zisiwe sehemu ya uchonganishi na kiongozi wa nchi kwani wataharibu taswira ya nchi.

Alisema ni vizuri asasi hizo kuepukana na siasa katika kazi zao kwa kuwa hazina maslahi wala matokeo chanya.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Isack Joseph (katikati), akizindua jarida la Taasisi ya Wanahabari wa Usaidizi wa Jamii ya Pembezoni (MAIPAC) mapema wiki hii, litakalojikita katika kukusanya taarifa ya jamii ya Wahadzabe na Wamasai, jinsi wanavyotumia maarifa ya asili kulinda na kuhifadhi mazingira. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa MAIPAC, Mussa Juma na Mjumbe wa taasisi hiyo, Suzana Munuo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wavisihi vyama vya siasa wagombea uenyekiti

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wa maendeleo nchini, likiwamo Shirika la kiraia la TUSONGE CDO, linalotoa elimu ya uraia kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa,vijiji na vitongoji utakaofanyika mwaka huu, limevisihi vyama vya siasa, kutafuta namna bora ya kuwapata wagombea wa nafasi za uenyekiti.

TUSONGE CDO, limesema mfumo unaotumika sasa, hauwapi fursa wagombea wanawake kupenya kwenye mchakato ndani ya vyama, kwa kuwa nafasi za viti maalum zinawatupa nje ya ushindani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo linalofanya kazi zake katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Singida, Aginatha Rutazaa, alisema kuna mambo mengi wao kama wadau wa maendeleo wanayaona yanawarudisha nyuma wanawake kujitokeza kugombea nafasi hizo.

"Tunaloliona hasa ile mifumo ya vyama vya siasa, kuna kuwa na mambo mengi yanayorudisha nyuma akina mama kuingia katika mchakato wa uchaguzi na kuweza kufanikiwa.

Moja ule mfumo au taratibu za vyama vya siasa, unakuta kuna vigezo ni kama kwa makusudi vinaondoa akina mama nje.

"Watu kama wale wanaoitwa 'wajumbe' waangaliwe upya. Hao ndani ya vyama wakati mwingine hawatendi haki, kwa sababu kuna mgombea mmoja ana maslahi na anajua namna ya kucheza nao ili kupata kura zao na kuwashinda wengine hata kabla ya kura za maoni.

...Yale makundi ya pembezoni, utaratibu mzima unavyoandaliwa wa kuandikisha wapiga kura kuna makundi yanayosahaulika. Makundi kama ya watu wenye ulemavu unakuta ile mifumo iliyoandaliwa haiangalii kwa upana kiasi hicho."

Rutazaa ameiomba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Tume Huru ya Uchaguzi nchini (INEC) kuboresha mahitaji ya jamii ya watu wenye ulemavu katika uchaguzi huo na ule mkuu wa mwakani.

Mwanaharakati huyo, Rutazaa alifafanua, "Kuna watu awanaohitaji maandishi ya nukta nundu, kuna watu wanaohitaji labda tafsiri ya mkalimani katika zoezi zima, unakuta havipatikani.

"Lakini hata miundombinu ambayo inatumika katika kuendeshea zoezi lile, mingi unakuta ni ofisi za serikali ngazi za kata na kwenye ngazi za mitaa, vijiji na unakuta majengo yake ni yale yaliyojengwa siku za nyuma hayafikiki kwa watu wenye ulemavu wanaotumia viti mwendo.

"Tuliiomba serikali hayo yazingatiwe na zoezi lile linajumuisha kila mtu, basi maeneo na ule ujumuishaji wa dhati uangaliwe ili kila mtu aweze kuingia katika mchakato huo."

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Umaarufu wa pilau ulivyopungua, soda nayo sasa siyo mpaka sikukuu

## -Ukipikwa wali kuoga mapema!

**Na Adam Fungamwango**

NI kama tunaishi katika dunia mbili tofauti. 'Watoto' wa mwishoni mwa miaka ya 1990 na 2000 hawawezi kunielewa hapa. Wengine hawatoamini. Wengine watacheka na kushangaa kwa pamoja.

Lakini ukweli ni ule ule kwamba tulioishi miaka ya 1970 ambao tupo hadi leo ni kama tunaishi katika dunia mbili tofauti.

Eti leo mtoto wangu akitaka soda unakwenda kumnunulia kwenye duka la jirani, tena anachagua soda gani anataka. Wakati mwingine zinakuwa kwenye friji kabisa. Akitaka anakwenda mwenyewe kufungua, anajisevia.

Mama yake anapika pilau siku akijisikia. Iwe Jumatatu, Jumanne, Jumatano, yaani siku na muda wowote ule ambao yeye au watoto watakapokuwa na hamu ya pilau.

Wanapokuwa wanakula mimi nawatazama sana, halafu naona kama wanaichukulia poa hivi.

Wanakula taratibu, wakati mwingine mpaka wasikie sauti ya mama yao akiwahimiza, 'asinyanyuke mtu hapo hadi muumalize.''

Baada ya hapo nikafanya uchunguzi mdogo tu, nikagundua siyo kwangu tu, bali kwa sasa ndivyo ilivyo.

Umaarufu au uadimu wa pilau na kinywaji soda kwa sasa havipo tena. Kwa sababu vinapatikana muda wote.

Nchi imeendelea, imekua, makampuni ya vinywaji yamekuwa mengi kiasi kwamba vinapatikana muda wowote na wakati wowote.

Vyakula vimekuwa vikipatikana kipindi chote cha mwaka, ingawa kuna wakati mchele unaadimika, lakini haiwezi kuwa kama kipindi hicho.

Sasa ngoja tu niwaambie vijana wa miaka ya sasa kuwa enzi hizo, kula wali tu, achilia mbali pilau.

Jamani tulipotoka mbali sana, huwa nashangaa tu kumsikia mtu akisema maendeleo hakuna.

Siyo kama zamani hakukuwa na raha, au watu hawakula maisha kama ya sasa, ila kilitokea kipindi kigumu na hii ni baada ya Vita Kagera.

Baada ya neema ya Uhuru mwaka 1961, wananchi wakila maziwa na asali, ilitokea vita kati ya Tanzania na Kagera iliyopiganwa kuanzia Oktoba 30, 1978 hadi Aprili 11, 1979.

Mwanzilishi wa vita hivyo alikuwa Raia wa Uganda wakati huo, Iddi Amini Dada aliyedai eneo la Mto Kagera na baadhi ya vitongoji ni mali ya Uganda, na hakuongea kwa maneno alivamia ardhi hiyo.

Tanzania ikalazimika kuingia vitani kukomboa eneo lake, lakini hata baada ya kufanya hivyo, ikaamua kumfundisha adabu Amin ndani ya mipaka yake, kiasi cha kuamua kukimbilia nchini Libya.

Tanzania, chini ya Rais wa Kwanza, Julius Nyerere, iliibuka kidedea.

Hata hivyo athari za vita hiyo ilisababisha uchumi wa nchi kuyumba, ndipo hali ya upatikanaji vyakula, nguo, mahitaji mengine muhimu ukawa mgumu.



Ndiyo kikaja sasa kile kipindi nilichokusudia kukisema, kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Kunywa soda ilikuwa ni mpaka siku za sikukuu au mgeni aje nyumbani. Soda ilikuwa anasa kwa sababu haikupatikana kirahisi sana madukani, na bei yake kwa wakati huo ilikuwa kubwa ukilinganisha na sasa kwa thamani. Pamoja na kwamba ilionekana ndogo ukiitaja lakini kwa wakati huo si wazazi wengi ambao walimudu, tofauti na bei sasa na upatikanaji wake.

Ikifika sikukuu ndipo baba anawanunulia watoto wake soda. Au kuwe na sherehe jirani, kwa ndugu jamaa ndipo unakunywa. Wakati mwingine labda mgeni akija nyumbani, anywe akubakishie, au akumiminie kwenye glasi. Kama mgeni mwenyewe 'kauzu' au mzazi kakufukuza ili usidoee, ndiyo umenoa hivyo.

Pilau watu waliila siku kwenye sherehe au hafla mbalimbali, mwenye misiba, au siku za sikukuu.

Tuliokuwa watoto nyakati hizo ni kwamba ikifika sikukuu furaha inakuwa ni kununuliwa nguo mpya pamoja na kula pilau. Yaani kula kama hivi sasa siku yoyote ile, thubutu! Yaani kwa mwaka unaweza kuhesabu umekula mara ngapi. Sehemu gani lilikuwa tamu sana, au nyama nyingi, uwezo wa kukumbuka tulikuwa nao kwa sababu wala si mara nyingi.



Wakati watoto wa sasa wakila ubwabwa asubuhi mchana na usiku, enzi hizo kula wali ilikuwa mbinde.

Kwanza hata ukipatikana haiiwi mchana. Jioni, tena siku hiyo watoto wanaoga mapema na nyumba ambayo wanakula wali inakuwa simulizi. Du! Watu tumetoka mbali jama, msituone hivi!

**Tuma meseji 0716 350534**

## HABARI KIMATAIFA

# Miili 60 yapatikana kwenye vifusi Gaza

**GAZA,** PALESTINA

MAOFISA katika eneo linalodhibitiwa na Hamas wamesema zaidi ya miili ya watu 60 imepatikana kwenye vifusi katika viunga vya mji wa Gaza baada ya jeshi la Israel kufanya mashambulizi katika mji wa Gaza.

Zoezi la kutafuta miili na watu walionusurika lilifanyika baada ya jeshi la Israel kutangaza kusitisha operesheni yake katika eneo hilo.

Wakati hayo yakijiri, Rais wa Marekani Joe Biden alisema mazungumzo juu ya mpango unaowezekana wa kusitisha mapigano yanapiga hatua.

Israel imevurumisha makombora katika mji wa Gaza kwa wiki moja mfululizo, hatua ambayo wakazi wameitaja kama vita vikali zaidi tangu mashambulizi yalipoanza.

Israeli imekuwa ikiishambulia Gaza kwa muda wa miezi 10 katika vita ambavyo vimeharibu maeneo na kuua zaidi ya Wapalestina 38,000, kulingana na mamlaka za afya huko Gaza.

Msemaji wa Ulinzi wa Raia, Mahmud Bassal, alisema asilimia 85 ya majengo yameharibiwa na kulitaja eneo la Shujaiya kama la maafa.

Kulingana na mamlaka ya Palestina, takriban watu sita waliuwawa Alhamisi katika mashambulizi ya anga ya yaliyolenga jiji la Gaza na wengine 19 katika maeneo mengine ya Ukanda wa Gaza.

Huduma ya dharura ya raia imeripoti kwamba miili ya Wapalestina wasiopungua 30 waliouawa imetawanyika kwenye barabara zisizoweza kufikiwa katika Jiji la Gaza.

Mapigano hayo yalipamba moto kutoka kaskazini hadi kusini mwa eneo la pwani huku mazungumzo yakiendelea kufikia makubaliano ya kusitisha mapigano na kuwaachilia mateka.

Jeshi la Israel lilisema wanajeshi wanaendelea na operesheni mjini Rafah ambao unapakana na nchi ya Misri.

Katika taarifa yake lilidai kuwauwa wanamgambo wengi katika mapambano ya ardhini na mashambulizi ya anga, na kwamba wameharibu miundombinu ya kigaidi katika eneo hilo. Rais Joe Biden juzi alisema mpango wake wa kusitisha mapigano Gaza umekubaliwa na Israel na kundi la Hamas. Hata hivyo alikiri kuwa bado kuna mapengo ya kuziba.

"Wiki sita zilizopita, niliweka mpango wa kina kwa maandishi. Uliidhinishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, na kundi la G7. Mfumo huo sasa unakubaliwa na Israel na Hamas. Haya ni masuala magumu na yenye changamoto. Bado kuna mapungufu," alisema Biden. Mazungumzo hayo ambayo yanaongozwa na nchi za Marekani, Misri na Qatar yanalenga juu ya mpango wa hatua tatu.

**DW**



Taswira mpya ya mji wa Gaza ukionekana kama magofu baada ya mashambulizi makali ya jeshi la Israel juzi. **PICHA: REUTERS**

# Mkuu wa polisi Kenya ajiuzulu

**NAIROBI,** KENYA

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini Kenya, Inspekta Jenerali, Japheth Koome, amejiuzulu kufuatia maandamano yaliyoambatana na ghasia na kusababisha zaidi ya watu 40, kuuawa.

Awali, mashirika ya kutetea haki za binadamu yalishutumu polisi kwa kuwapiga risasi waandamanaji, kuwaua, kuwakamata kiholela na kuwateka nyara.

Maandamano hayo yalianza nchini humo katikati ya mwezi uliopita kupinga mapendekezo ya nyongeza ya kodi katika muswada wa fedha wa 2024.

Waandamanaji hao walivamia majengo ya bunge muda mfupi baada ya wabunge kupitisha mswada huo tata. Hatua hiyo ilimfanya Rais William Ruto kukataa kusaini katika jitihada za kuyazima.

Pia juzi alivunja baraza la mawaziri ili kutekeleza madai ya waandamanaji hao yaliyoongozwa na vijana wanaojiita Gen Z. "Rais William Samoei Ruto, ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, amekubali kujiuzulu kwa Eng. Japheth N. Koome, kama mkuu wa polisi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Wakati huo huo, miili kadhaa ya watu waliouawa imeokotwa ikiwa imewekwa kwenye mifuko na kutupwa katika eneo la dampo karibu na kitongoji duni cha Mukuru Kwa Njenga jijini Nairobi.

Kulingana na Capital News, wanaharakati waliogundua maiti hizo baadhi zilikuwa zimekatwa viungo.

Polisi walifika kwenye eneo la tukio kusimamia zoezi la utafutaji wa miili mingine.

Hata hivyo, mamlaka huru ya Usimamizi wa Polisi (IPOA) ilitoa taarifa ya kupokea malalamimiko 10 kuhusu visa vya kukamatwa, kutekwa nyara na kupotea baada ya maandamano ya kupinga Muswada wa Fedha 2024.

IPOA ilisema malalamiko manane kati ya hayo, waathirika walipatikana wakiwa hai, mmoja bado hajulikani alipo huku mmoja alipatikana akiwa amefariki dunia.

**BBC.**

# Wafungwa hatari watoroka Gereza lenye ulinzi mkali

**NIAMEY, Niger**

WAFUNGWA kadhaa wanasakwa baada ya kutoroka kwenye gereza lenye ulinzi mkali la Koutoukalé, karibu na mji mkuu Neamey nchini Niger.

Tukio hilo limetokea juzi na serikali ilitangaza sheria ya kutotoka nje usiku katika eneo hilo.

Katika tangazo lililotolewa kwa njia ya redio, Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi hiyo ilielezea kuwa gavana wa eneo la Tillaberi alitaarifu kutoroka kwa wafungwa kutoka gereza la Koutoukalé, linalopatikana kilomita 50 kutoka mji mkuu wa Neamey.

Wizara hiyo haikueleza idadi ya wafungwa waliotoroka ndani ya gereza hilo lenye ulinzi mkali zaidi nchini humo na ambako wafungwa hatari wanazuiliwa, hasa wapiganaji wa kijihadi waliokamatwa kwenye uwanja wa vita.

Taarifa hiyo ya serikali iliomba vikosi vya usalama kuongeza umakini wao katika mfumo mzima wa usalama.

Mamlaka ya eneo la Tillabéri, kwa upande wake, ilitangaza sheria ya kutotoka nje usiku katika eneo hilo siku ya Alhamisi jioni na kupiga marufuku watu kutembea kwa miguu, pikipiki na magari magari kuanzia saa 3:00 usiku.

Kulingana na tovuti ya Niger ya Actuniger.com, viongozi wa magaidi ni miongoni mwa wafungwa waliotoroka.

Katika msako wa wafungwa hao, wizara iliomba mamlaka ya Tillaberi kuhusisha machifu wa kimila na viongozi wa kidini.

Pia iliwataka kuongeza ufahamu miongoni mwa watu katika kumshuku mtu yeyote wanayemuona ni mgeni.

Eneo la Tillaberi, linafahamika kama eneo la mipaka mitatu kutokana na kupakana na nchi za Mali na Burkina Faso, limekuwa maficho ya wanajihadi wa kundi la Sahel wanaohusishwa na Islamic State na Al-Qaeda.

Gereza la Koutoukalé lilikabiliwa na mashambulizi mawili katika siku za hivi karibuni.



Raia wa China, Xia Xiaomao, akiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam juzi, akisubiri kusomewa shtaka la kufanya biashara ya kubadilisha fedha za Kigeni bila kuwa na leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania, ambapo alihukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni mbili au miaka 5 jela ikiwa ni pamoja na kutaifishwa kiasi cha shilingi za Kitanzania zaidi ya milioni 16 na Dola 64,255. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Marathon ya CRDB kuvuna bilioni 2/- Burundi, DRC

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zimepongeza Benki ya CRDB kwa kuanzisha mbio za marathon katika nchi zao, waandaaji wakilenga kukusanya Sh. bilioni mbili.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Balozi wa Burundi nchini, Leontine Nzeyimana, na Mwakilishi wa Balozi wa DRC nchini, Patrice Tshekoya, wakisisitiza umuhimu wa mbio hizo katika kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi hizo.

"Benki ya CRDB imeonesha ni kwa namna gani si tu iko kibiashara bali pia inajali jamii. Tunawashukuru kwa moyo wenu huu wa kujitoa.

"Kwa miaka zaidi ya 10 ambayo benki hii imekuwa Burundi imekuwa na mchango mkubwa katika kuchochea maendeleo. Burundi na Tanzania ni ndugu, na Benki ya CRDB Burundi ipo nyumbani, hivyo hata marathon hii pia imefika nyumbani," alisema Balozi Nzeyimana.

Akizungumza kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Said Shaibu Mussa, alipongeza Benki ya CRDB kwa uamuzi wa kuandaa marathon katika nchi tatu, akisema jitihada hizo zinaendana na juhudi za Serikali ya Tanzania kuboresha uhusiano wa kidiplomasia na nchi jirani.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Group, Abdulmajid Nsekela, alisema upanuzi wa marathon ya benki yao katika nchi za DRC na Burundi unakwenda sambamba na malengo ya benki ya kujitanua kikanda na kuchochea maendeleo barani Afrika.

Nsekela alisema benki hiyo imejipanga kikamilifu kusaidia kuweka mazingira wezeshi na kuwawezesha wananchi katika nchi inapotoa huduma kunufaika na fursa malengo ya Afrika Tuitakayo 2063.

"Benki ya CRDB imefanikiwa kufikia mafanikio makubwa katika nchi za DRC na Burundi kutokana na uhusiano mzuri baina ya Tanzania na nchi hizo, yakichagizwa na uongozi mahiri wa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Burundi, Evarist Ndayishimiye na Rais wa DRC Congo, Félix Tshisekedi," alisema Nsekela.

Malengo ya msimu wa tano wa CRDB Bank Marathon ni kusajili wanajeshi wa kusambaza tabasamu (washiriki) zaidi ya 8,000 na kukusanya zaidi ya Sh. bilioni mbili.

Katika msimu huu, benki hiyo inatarajia kuanza jijini Lubumbashi, DRC Agosti 4 kisha kuelekea jijini Bunjumbura, Burundi Agosti 11 kabla ya kurudi Dar es Salaam Agosti 18.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa ambaye ndiye Kamanda wa Jeshi la Kusambaza Tabasamu (JLKT) la CRDB Bank Marathon, alisema mbali na makundi ambayo yamekuwa yakinufaika na mbio hizo ikiwamo watoto wenye maradhi ya moyo na kinamama wenye ujauzito hatarishi na fistula.

Alisema kuwa mwaka huu sehemu ya fedha zitakazokusanywa zitakwenda kusaidia jitihada za kujengea uwezo vijana nchini.

"Takwimu za Sensa ya Mwaka 2022 zinaonesha vijana ni asilimia 75 ya Watanzania wote. Inakadiriwa kuwa takriban vijana milioni moja wanaingia katika soko la ajira la Tanzania kila mwaka.

"Vijana wanapowezeshwa, wanaweza kuwa nguvu ya kubadilisha jamii kwa njia chanya, kuchangia kikamilifu katika ukuaji kiuchumi, kukuza uvumbuzi, na kujenga mazingira endelevu kwa ajili ya siku zijazo," alisema Tully.

Katika utekelezaji mpango huo wa uwezeshaji vijana kupitia CRDB Bank Marathon, Benki ya CRDB pia imekabidhi msaada wa fedha kwa timu ya Taifa ya Olympic kushiriki katika mashindano ya Olimpiki yatakayofanyika Paris, Ufaransa kuanzia tarehe 26 Julai hadi 11 Agosti 2024.

Akikabidhi hundi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Group, Nsekela alisema, "Uwezeshaji timu hiyo ya Taifa ya Olimpiki ni hatua muhimu ya kuwaweka vijana katika ramani ya kimataifa, ikitoa njia ya mafanikio kwao binafsi, familia zao na jamii kwa ujumla."

Katika ripoti iliyowasilishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, mnaelezwa kuwa kwa misimu minne iliyopita, mbio hizo zilikusanya Sh. bilioni 2.7 ambazo zilielekezwa katika kusaidia upasuaji kwa watoto zaidi ya 300 wenye maradhi ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kinamama wenye ujauzito hatarishi zaidi 150 katika Hospitali ya CCBRT, ujenzi wa Kituo cha Mawasiliano Taasisi ya Kansa ya Ocean Road (ORCI), ujenzi wa Kituo cha Afya ya Mama na Mtoto Zanzibar, na kampeni ya utunzaji mazingira ya 'Pendezesha Tanzania'. Zaidi ya wakimbiaji 12,000 walishiriki wakiwa sehemu ya Jeshi la Kusambaza Tabasamu (JLKT).

# Raia wa China akwepa kifungo miaka mitano

**Na Grace Gurisha**

RAIA wa China, Xie Xiaomao, maarufu Celine, amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni mbili au kwenda gerezani kutumikia kifungo cha miaka mitano baada ya kupatikana na hatia kwa kosa la kufanya biashara ya kubadili fedha za kigeni bila ya kuwa na leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Adhabu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam, Rahim Mushi, baada ya mshtakiwa kusomewa shitaka na kukiri kutenda kosa hilo.

Hakimu Mushi alisema kabla ya kutoa hukumu hiyo, amezingatia hoja za pande zote mbili ikiwamo mshtakiwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza.

"Mshtakiwa huyu hakuisumbua mahakama, kwani alikiri shtaka pamoja na hoja za awali alizosomewa, hivyo ameokoa muda wa mahakama kusikiliza kesi hii kama angekana shtaka," alisema Hakimu Mushi.

Alisema mshtakiwa baada ya kukiri kosa lake, mahakama inamtia hatiani katika kosa la kufanya biashara bila kibali cha BoT, kwa hiyo atatakiwa kulipa faini ya Shilingi milioni mbili na akishindwa atatumikia kifungo cha miaka mitano.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alifanikiwa kulipa faini na kuachiwa huru na mahakama.

Mahakama hiyo pia, imetaifisha Sh. 16,797,000 na Dola za Marekani 64,255, Yuan 500 alizokamatwa nazo kuwa mali ya Serikali ya Tanzania.

Awali, akimsomea shtaka lake, Wakili wa Serikali Mwandamizi Christine Joas, alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo kati ya Januari hadi Mei 16, mwaka huu, katika duka kubwa (Supermarket) la Peninsula, eneo Oysterbay, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Inadaiwa kuwa, mshtakiwa akiwa eneo hilo alikutwa akifanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni bila kuwa na leseni kutoka BoT.

Inadaiwa kuwa, Mei 16, mwaka huu, mlalamikaji aliweka mtego na kumpa msiri fedha za Tanzania aende kuzibadilisha kwa mshtakiwa ambazo zilikuwa noti 281 za Sh. 10,000, sawa na Sh. milioni 2.81.

Alidai kuwa msiri alikwenda na bila wasiwasi mshtakiwa alibadili fedha hizo, alitoa taarifa polisi ambao walifika na kumkamata mshtakiwa.

"Baada ya kukamatwa upekuzi ulifanyika na kukutwa na fedha hizo za mtego, noti mbalimbali za kigeni zikiwamo noti 627 za Dola za Marekani 100, noti 22 za Dola 50 (noti 7), za Dola 5 (noti 18), za Dola 10 (noti 102), za Sh. 10,000 na fedha za China Yuen 500," alidai.

Inadaiwa kuwa noti 281 za Sh. 10,000 alizokamatwa nazo mshtakiwa zilifanana na fedha za mtego na baada ya upekuzi fomu ya kukamata mali ilijazwa, mshtakiwa na polisi waliokuwa katika upekuzi walitia saini.

Mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani na kufunguliwa kesi hiyo.

**Baada ya kukamatwa upekuzi ulifanyika na kukutwa na fedha hizo za mtego, noti mbalimbali za kigeni zikiwamo noti 627 za Dola za Marekani 100, noti 22 za Dola 50 (noti 7), za Dola 5 (noti 18), za Dola 10 (noti 102), za Sh. 10,000 na fedha za China Yuen 500.**


HADITHI

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-**21**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




"Sasa nikwambie kitu, hapa inaonekana pamoja na kwamba watu wengine wameshiriki hili, lakini mpenzi wako alikuwa anatakiwa na mtu mmoja tu ambaye ndiye tunamsaka." "Nadhani Dokta."

"Na yeye ni mtu mwenye uwezo wa kipesa, tajiri au mwenye wadhifa hivi, aliyekuwa akitaka kutumia nguvu yake kukunyang'anya mpenzi na aliposhindwa akafanya hivyo na sasa anajaribu kuficha ushahidi kwa gharama zozote." "Sawa kabisa Dokta." "Sasa ulizifahamu namba hizo zote ni za nani?"

"Kusema kweli namba za meseji zangu mbili ni tofauti na za kwenye simu ya Mariamu pia ni mbili tofauti. Na kwa bahati mbaya nilijaribu kujifanya kama natuma pesa kwao, lakini mtandao ulijibu kuwa hazikuwa zimesajiliwa." "Da pole sana. Hawa watu walikuwa wamejipanga hasa." "Sasa kuna ndugu yangu mmoja, mdogo wangu, yeye ni askari polisi kitengo cha IT, suala lako limenigusa sana ilibidi nimuelezee hata kama wewe mwenyewe ulikuwa hupendi, lakini nimefanya hivyo wakati mwingine kwa ajili tu ya msaada. Ameniambia kama namba zipo basi unipe nimpelekee na jambo la kwanza atakalolifanya ni kujua zimesajiliwa wapi na waliozisajili ni akina nani."

"Ha! Dokta, utakuwa ni msaada mkubwa kwangu. Unajua mwanzoni sikukuamini kabisa nilipojitambulisha kwako, nikajua unaweza kuniuza kwa wanaonitafuta, lakini mpaka umefikia huko, ina maana kweli umemua kunisaidia." Kamal aliongea kwa furaha na bashasha, kwani alijua sasa hayupo peke yake. Kuna mtu amemua kumpigania na jambo hilo gumu linalomkabili.

Mazungumzo muhimu yalikuwa yameishia hapo, na ilikuwa kaba gari halijarejea tena eneo la Kariakoo makutano ya Uhuru na Msimbazi.

"Da ila jamaa wewe kama mpelelezi, yaani hadi hospitali umehama, ukaona kwa sasa nimejua, ukawa huniamini tena." Daktari akachombeza baada ya mazungumzo kumalizika.

Kamal akacheka. "Ni kweli, kwa sababu huwezi kujua mzuri na mbaya wako, labda mpaka uwe na ungalau uhakika asilimia nyingi kama hivi sasa. Nianza kukuamini. Kwa sababu hadi kufikia hatua hiyo, nimekubali uko na mimi."

"Sasa mbona mwanzo hukuniamini?" "Kwani aliopindisha ripoti ya mauaji, si madaktari kama wewe?" Kamal naye aliuliza swali badala ya kujibu, halafu wote wakaangua vicheko.

"Sasa utarudi uendelee kuishi hospitali?" Dokta Shija akauliza tena. "Hapana, nimepata sehemu nyingine ya kukaa. Siyo kwamba bado sikuamini, ila haitokuwa vyema tena kuhama tena nilipo." Akadanganya. Ukweli ni kwamba hakutaka kurejea tena kwenye ile zahanati kwa sababu mara kwa mara imekuwa ikipokea watu ambao baadaye wanaweza kumtilia shaka, tofauti na kule kwenye mabehewa chakavu Kurasini, ambapo watu anaokutana nao ni walinzi wasiozidi watatu tu wanaofanyiana zamu na tayari wameshamzoea.

"Wewe bwana huwezi kurudi tena Kigoma.Umeshazoea Dar." Huwa wanamtania mara kwa mara kutokana na uongo wake wa mwanzo kabisa kuwa alimfuata ndugu yake Dar akitokea Kigoma, lakini alipofika simu yake ilikuwa imezimika na hakujua pa kwenda kwa sababu ni mgeni.

Walimpa sehemu ya kulala kwenye moja ya behewa chakavu, na imefika mwezi sasa, jamaa yao hajampata mwenyeji wake na anaendea kuwepo hapo.

Haikuwashughulisha walinzi hao, baada ya kubaini hakuwa mtu mbaya, badala yake ni mcheshi ambaye hupiga naye stori na wakati mwingine huwaletea zawadi mbalimbali ya vyakula na vitafunwa.

Akawadanganya kuwa kwa sasa anafanya vibarua sokoni Kariakoo, ambavyo humpatia vijisenti na kujikimu.

Hakuna yoyote aliyejua kuwa anayeishi pale ni mtuhumiwa wa kesi ya mauaji ya mpenzi wake, ambaye mara kwa mara picha yake hutolewa kwenye vyombo vya habari.

Kwa bahati nzuri picha ile iliyokuwa inatolewa aliipiga zamani kidogo, ambapo kwa kiasi fulani wala haifanani naye kwani alikuwa na nywele nyingi tofauti na sasa ambapo huzikata makusudi na kujitahidi kubadisha ili asifanane sana na anavyotoka kwenye gazeti.

Kazi yake kila asubuhi ilikuwa ni kwenda kwenye vyoo tofauti vya kulipia, anaoga na kubadilisha nguo, na hata akirejea inakuwa hivyo hivyo.

Huvaa nguo chakavu anapotoka kwenye behewa bovu, lakini huzibadilisha anapokuwa kwenye shughuli zake huko, akiwa amebadilishia kwenye moja ya mabafu na vyoo vya kulipia vilivyozagaa katikati ya jiji.

************************

Siku tatu baadaye, akiwa anatoka sehemu aliyofanya makazi yake, alisikia simu inaita. Akaingiza mkono mfukoni, akaangalia jina, lilikuwa la Dokta Shija.

"Ni hivi, njoo pale pale makutano ya Uhuru na Msimbazi nina salamu zako kutoka kwa ndugu yangu. Ni nzuri, nadhani zinaweza kutupa mwanga kama zitafanyiwa kazi," alisema.

**Kule kule karibu na nyumba kwa marehemu mpenzi wangu?" "Ndiyo, halafu cha kushangaza na kufurahisha kwa upande wetu, ni kwamba zote nne zimesajiliwa sehemu moja.**

Haraka, Kamal alifanya kama alivyoagizwa. Akakutana na Dokta ambaye kama kawaida, alimwambia ainge kwenye gari lake.

Baada ya salamu, wakaanza kutaniana na baadaye akamwambia alichokuwa anamuitia.

"Ndugu yangu, mdogo wangu ambaye nilikwambia ni askari kitengo cha IT, amenisaidia huku na huku, kahainga kwa kuwashirikisha wenzake, hatimaye wamegundua kuwa namba hizi ni kweli hazina majina ya watu waliosajini, lakini zimesajiliwa maeneo ya Tabata Bima."

"Kule kule karibu na nyumba kwa marehemu mpenzi wangu?" "Ndiyo, halafu cha kushangaza na kufurahisha kwa upande wetu, ni kwamba zote nne zimesajiliwa sehemu moja." Akajibu Dokta.

"Duh!" Akashangaa Kamal. "Halafu zimesajiliwa muda huo huo kwa wakala mmoja anaitwa Shida Mrosso." Akasema akimtazana Kamal kwa natasamu halafu akaongeza. "Kaniambia hivi, unaweza kwenda na kumuuliza waliosajili pale walisajili kwa majina gani. Hawawezi kuongopa kwa sababu huwezi kusajili bila kitambulisho cha Nida." "Nashukuru sana Dokta Shija kwa msaada wako unaoendelea kunipa wewe na mdugu yako afande." "Usijali Kamal, nitakusaidia mpaka mwisho kwa sababu niliapa wakati tunafanya uchunguzi wa mwili wa mpenzi wako mara ya pili, nikajisemea moyoni kuwa kama ningemfahamu huyu kijana alinayesingiziwa mpenzi wake kuna vitu ningemsaidia, kwa sababu ukweli ni kwamba hajaua, na uthibitisho ni jinsi nguvu ya fedha ilivyotumika kufika ukweli kuwa ameuawa, ionekane amengua kwa presha, ndugu na watu walivyokataa, tukaingia sisi tukachunguza na kugundua kuwa ameuawa, halafu ikatumika tena nguvu ya pesa kumtafuta muuaji feki, huku wale halisi wakilindwa."

"Nakuhakikishia Dokta ninakuamini na tutakuwa nawe pamoja. Kazi hii nitaifanya kesho, nitakwenda Tabata Bima kituoni ambapo umesema ndipo eneo lake lipo. Naweza kuifanya kazi hii, nitapata majina ya watu hao. Nadhani tukiyapata tutakuwa kwenye njia sahihi ya kuelekea kwa muuaji au wauaji." "Swadakta, tena aliniuliza anaweza kufanya kazi hii, nikamwambia jamaa mwenye mienendo yake kama askari mpelelezi, kwa hiyo kwake kazi hii ndogo sana, akacheka."

Alipomaliza Dokta na Kamal nao wakaangua vicheko.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SINGIDA BLACK STARS YAPANIA LIGI KUU BARA

**Na Faustine Feliciane**

KLABU ya Singida Black Stars imepania kufanya vizuri msimu ujao wa ligi kuu baada ya kukamilisha usajili wa golikipa wa timu ya taifa Siera Leon , Muhammed Nbalie Kamara.

Golikipa huyo aliiambia Nipashe kutokea Siera Leon kuwa anatarajia kutua nchini leo tayari kujiunga na kikosi cha timu hiyo baada ya kila kitu kukamilika.

**Kamara, alimthibitishia mwandishi wa habari hizi kuwa tayari yupo kwenye maandalizi ya kuja nchini leo.**

“Ni kweli nakuja Tanzania kujiunga na Singida Black Stars, kila kitu kipo sawa na tumemalizana, kilichobaki ni mimi kuja huko,” alisema Kamara.

Aidha, msemaji wa Singida Black Stars Hussein Massaza, aliithibitishia Nipashe kuwa mchezaji huyo ni mali yao na atakuwepo kwenye kikosi chao msimu ujao.

“Ni kweli kaka, atakuwa sehemu ya kikosi chetu msimu ujao, taarifa nyingine tutazitoa baada ya kumtangaza rasmi,” alisema Massaza.

Kamara ambaye kwa sasa ana miaka 25 alianza kuichezea klabu ya kwao ya FC Johansen ambapo alitumika kwa msimu mmoja na baadae mwaka huo akajiunga na klabu ya East end Lions alipofuzu kwa miaka mitatu kabla ya Horoya FC ya Guinea kumsajili mwaka 2022 kwa mkataba wa miaka miwili unaomalizika mwaka huu.



Vijana wakifanya mazoezi ya mpira katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## John Bocco wa kwanza mazoezini JKT Tanzania

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Simba, John Bocco amekuwa wa kwanza kuripoti mazoezini wakati kikosi cha JKT Tanzania kikikutana kuanza mazoezi ya msimu wa mashindano msimu ujao, huku klabu hiyo ilimsajili anayesaidiana naye katika kupachika mabao, Charles Ilamfya.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Masau Bwire, amesema kitendo hicho kinaonyesha kuwa Bocco ni mchezaji mwenye nidhamu na ndiyo maana hawakufanya kosa kumleta kwenye kikosi hicho.

“Niseme tu kuwa kikosi kimeanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao, lakini nahodha wetu mpya, Bocco, amekuwa wa kwanza kuwasili mazoezini na hii inaonyesha jinsi gani alivyokuwa mchezaji mwenye nidhamu. Angalia, mchezaji staa hapa nchini kama yeye, siku ya kwanza tu mazoezini akafika, tena akiwa mchezaji wa kwanza, si rahisi kulikuta hili kwa wachezaji wengi wa Kitanzania, anastahili sifa na hii inaonyesha ni kwa nini tumemleta kwenye kikosi chetu,” alisema Masau.

Bocco, ambaye pia alikuwa nahodha wa kikosi cha Simba, alikuwa mchezaji wa kwanza kupewa mkono wa kwaheri, lakini haikumuacha hivi hivi, bali ilimkabidhi timu ya vijana chini ya miaka 17 ili anoe.

## *DC Temeke azindua TIA Marathon 2024*

**Na Christina Mwakangale**

MKUU wa Wilaya Temeke, Sixtus Mapunda, amezindua mbio ‘marathon’ zitakazofanyika Oktoba, mwaka huu, zikilenga kutunisha mfuko kwa ajili ya ada wanafunzi walio na mahitaji maalumu kama vile watu wenye ulemavu.

Mapunda akizindua jana, mkoani Dar es Salaam, katika Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), alisema serikali inaungana na taasisi hiyo, kuhakikisha lengo la mbio hizo linatimia kwa kuungana na wadau mbalimbali.

“Niwapongeze TIA kwa kubuni mradi huu mkiwambuka hasa wenye mahitaji maalumu, ambao watatimiza ndoto zao, kwa kuwa na uhakika wa kusoma,” alisema Mapunda.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Prof. William Pallangyo alisema taasisi hiyo ilifanya utafiti na kubaini kwamba wapo wanafunzi ambao wanafanya vizuri katika masomo, huku baadhi yao walishindwa kumudu gharama za masomo.

“Mara nyingi baadhi ya wanafunzi huja ofisini kwangu wakiomba msaada wa kulipiwa ada, kama taasisi tukafikiria kuja na wazo hili.

“Kuna wanafunzi ambao ni mama vijana ‘young mother’s’ ambao wana familia na ni wadogo, ana mtoto anakaa nae hosteli, ana msaidizi, ana ndoto ya kusoma.,” alisema Prof. Pallangyo.

Alisema kauli mbiu ya mbio hizo ni ‘Run, Inspire and Support’ na kwamba pia lengo ni kuimarisha afya kwa wanafunzi na walimu, pia kukabiliana na Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs).

“Tunaandaa ‘TIA Marathon’ zitafanyika Oktoba 26, mwaka huu, tunalenga kuunga mkono serikali kwa namna anavyosaidia vijana kupata elimu, kuwasaidia ambao hawana uwezo na zitakuwa za kilomita tano, 10 na 21.”

## Wachezaji 124 wajitokeza michuano ya gofu

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

ZAIDI ya wachezaji 124 wakiwemo 52 wa mchezo wa kulipwa wamejitokeza kushiriki katika mashindano ya gofu ya kumuenzi nyota wa zamani wa timu ya taifa ya mchezo huo, Lina Nkya.

Mashindano hayo yanayofanyika kwa mara ya tatu, yameanza juzi kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Arusha na yanatarajiwa kumalizika kesho.

Mmoja wa wachezaji wa kulipwa anyeshiriki mashindano hayo, Nuru Mollel, alisema amejipanga vizuri kwa ajili ya mashindano hayo na ana matarajio makubwa ya kuibuka mshindi.

Aidha, aliwaasa watanzania hususani wapenzi wa mchezo huo kujitokeza kwa wingi kuona mchuano mkali uliopo.

“Nimejipanga vizuri hasa katika kuhakikisha naibuka mshindi katika mashindano haya, hata hivyo kushiriki kwenye jambo hili kwangu mimi ni fursa haşa ya kukutana na wachezaji wenzangu na kuendelea kubadilishana uzoefu,” alisema Mollel.

Naye mchezaji ambaye ni mshindi wa ridhaa mara mbili mfululizo kwenye mashindano hayo, Alli Sanzu, alisema mashindano hayo ya Arusha ni muhimu kwake kwa sababu ni ya mwisho kuelekea kwenye mashindano makubwa nchini Dubai.

Alisema amewekeza nguvu zake zote katika mashindano hayo kuhakikisha anafanya vizuri na kuibuka mshindi.

“ Mashindano haya yatakuwa sehemu ya maandalizi kwangu kabla ya kwenda Dubai kwenye mashindano mengine,” alisema Sanzu.

Mshindi wa kwanza katika mashindano hayo atapatiwa kikombe na fedha taslimu na zawadi nyingine.

Katika mashindano ya mwaka jana yaliyofanyika kwenye viwanja vya TPC, Moshi, Mollel aliibuka mshindi wa kwanza na kufuatiwa na Fadhili Nkya.

**Mashindano haya yatakuwa sehemu ya maandalizi kwangu kabla ya kwenda Dubai kwenye mashindano mengine.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEVES AGEUKA LULU

KLABU ya Paris St-Germain iko tayari kushindana na Manchester United katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka, 19 Joao Neves. ***(Le10Sport)***

### WILLIAMS FRESH BARCA

BARCELONA imefikia makubaliano ya kimsingi kwa mshambuliaji wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 21. ***(Sport)***

### DE LIGT HUYO MAN

KLABU ya Manchester United ina nia ya kukamilisha usajili wa beki wa Bayern Munich, Mholanzi Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 24, haraka iwezekanavyo baada ya Euro 2024. ***(Bild)***

### TAVARES NA ARSENAL

ARSENAL imekubali ofa ya mkopo kutoka kwa Lazio kwa beki wao wa pembeni wa Ureno, Nuno Tavares mwenye umri wa miaka 24 na kulazimika kumuuza kati ya pauni milioni 6. ***(Mirror}***

### CHELSEA HAINA MPANGO

CHELSEA haina nia ya kuanzisha kipengele cha kumnunua mshambuliaji wa Hispania, Dani Olmo, 26, katika klabu ya RB Leipzig kwa pauni milioni 50. ***(Sky Sports)***

### GREAVES SAFI IPSWICH

MLINZI wa kati wa England, Jacob Greaves, 23, amekamilisha matibabu yake ya kuhamia Ipswich Town kabla ya kuondoka kutoka Hull City. ***(Sky Sports),***

### RABIOT HURU

LIVERPOOL, Bayern Munich na Real Madrid huenda ndiko anakoelekea kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, ambaye ni mchezaji huru baada ya mkataba wake na Juventus kumalizika mwezi uliopita. ***(Calciomercato)***

### NKETIAH AWINDWA

MARSEILLE ianavutiwa na mshambuliaji wa Arsenal na England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 25. ***(Footmercato)***

### SIMONS AWANIWA

KLABU ya Bayern Munich inataka kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Xavi Simons, 21, kutoka Paris St-Germain. ***(Sky Sports)***

### YAKATAA KWA FOFANA

MONACO imekataa dau la euro milioni 30 kutoka kwa Nottingham Forest kwa ajili ya kiungo wa kati wa Ufaransa Youssouf Fofana, 25, ambaye amekubali makubaliano na AC Milan. ***(Fabrizio Romano)***

### PALHINHA SAFI BAYERN

KIUNGO wa kati wa Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 29, amekamilisha uhamisho wake kutoka Fulham hadi Bayern Munich. ***(Sky Germany)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# FA KUMBAKIZA SOUTHGATE KOCHA ENGLAND

**LONDON,** England

**Ni hata kama atakosa ubingwa wa Euro, huku mwenye msimamo wake ni...**

GARETH Southgate ataombwa kubakia kama kocha wa England hata kama timu yake itapoteza fainali ya Euro 2024 Jumapili, kwa mujibu wa BBC Sport.

**Mkataba wa Southgate unamalizika Desemba na kumekuwa na mwito mkubwa wa kumtaka aondoke mara tu kampeni ya kuwania ubingwa wa Ulaya kwa Simba Watatu hao utakapofika tamati mapema msimu huu wa joto.**

Tangu wakati huo, Southgate amekuwa kocha wa kwanza kuwaongoza vijana wa England kufuzu fainali mbili kuu tofauti, huku timu yake ikiingia katika hatua ya kukumbukwa ya mtoano hadi kufika Berlin.

Ripoti kadhaa za kuaminika zinadai kuwa FA sasa inamtaka Southgate kubakia katika wadhifa wake na kuiongoza England katika Kombe la Dunia la FIFA la 2026 nchini Canada, Mexico na Marekani.

Kufuzu kwa England hadi fainali ya Euro inasemekana kuthibitisha imani ya FA kwamba Southgate, ambaye aliteuliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2016, bado ndiye mgombea bora wa nafasi hiyo.

Lakini kuna uwezekano kwamba Southgate ataamua kuachana na jukumu lake mwenyewe baada ya fainali. Alikuwa akihusishwa na kibarua cha Manchester United kabla ya uamuzi wao wa kumbakisha Erik ten Hag, huku Thomas Tuchel, Mauricio Pochettino, Eddie Howe na Graham Potter wakipendekezwa kuchukua kiti hicho iwapo Southgate ataondoka.

Southgate amekuwa na nia ya kutozingatia mustakabali wake kabla na wakati wa Euro 2024, ingawa amezungumza kuhusu nia yake.

"Sote tunataka kupendwa, sivyo?," alisema baada ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Uholanzi.

"Kwa hiyo unapofanya kitu kwa ajili ya nchi yako na wewe ni Mwingereza mwenye kiburi, wakati haujisikii nyuma na wakati yote unayosoma ni ukosoaji, ni ngumu.

"Kuweza kusherehekea fainali ya pili ni maalum sana. Hasa kwa mashabiki wanaosafiri, sapoti yetu ya kusafiri ni ya kushangaza.

"Kiasi cha fedha wanachotumia kusafiri, kujitolea kufanya hivyo, kuweza kuwapa usiku kama huu. Nadhani tumewapa chache zaidi ya miaka sita iliyopita, kutoka Urusi na kuendelea. Ina maana kubwa. "

England itacheza na Hispania katika fainali ya Euro 2024 Jumapili kwenye Uwanja wa Olympiastadion mjini Berlin.

HABARI MICHEZO

# VAN DE BEEK SASA NI MALI YA GIRONA




**MANCHESTER,** England

DONNY van de Beek amekamilisha uhamisho wa kudumu kwenda Girona kutoka Manchester United, na hivyo kuhitimisha kipindi cha kusikitisha cha miaka minne pale Old Trafford.

Kiungo huyo wa kati wa Uholanzi, ambaye alijizolea umaarufu na kusifiwa kama sehemu ya kikosi cha Ajax ambacho kilifuzu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya 2019, amesaini mkataba wa miaka minne Girona ambako atakaa hadi mwaka 2028.

Van de Beek alihamia United kwa takriban pauni milioni 40 msimu wa joto wa 2020, kwa matarajio kwamba angesaidia kurudisha klabu iliyoimarika kuelekea kilele cha soka la Uingereza na Ulaya chini ya kocha, wa Ole Gunnar Solskjaer.

Lakini mapambano ya kujiimarisha, licha ya kufunga bao kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu, yalisababisha kuwa na muda mdogo wa kucheza.

Van de Beek alitumia kipindi cha pili cha kampeni ya 2021/22 kwa mkopo Everton, kabla ya hapo kujiunga na Eintracht Frankfurt, ambayo haikutumia chaguo la kumnunua, kwa miezi sita Januari 2024.

"Kila mtu katika United angependa kumtakia Donny kila la heri katika sura hii ijayo ya maisha yake ya soka. Atarejea Uingereza hivi karibuni, kwani Girona wana mechi za kirafiki za kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Newcastle United na Bournemouth mwezi ujao," taarifa kutoka kwa klabu yake ya zamani ilisema.

Van de Beek alikuwa tayari amezungumza kuhusu kuondoka kwake katika ujumbe kwa mashabiki mapema wiki hii.

# Man City, Barca zaongezewa muda kwa Olmo



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City na Barcelona zimeongezewa muda ili kuanzisha kipengele cha kutolewa katika mkataba wa Dani Olmo wa RB Leipzig, ripoti zimefichua.

Olmo amekuwa akiwindwa na klabu kadhaa vya juu msimu huu wa joto, ikiwa ni pamoja na Barcelona, ambayo imetoa ofa ya mdomo kwa kiungo huyo, huku City pia ikimfuatilia.

Matatizo ya kifedha ya Barcelona yanamaanisha haiwezi kumudu kipengele cha kutolewa cha Olmo cha euro milioni 60 na hiyo inaweza kufungua njia kwa City kupata saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa ofa nzuri zaidi.

Safu ya kiungo ya City inahitaji kuimarishwa huku kukiwa na uvumi unaoendelea kuhusu hatima ya Kevin De Bruyne, ambaye mkataba wake unamalizika 2025 na Bernardo Silva.

Kulingana na Fabrizio Romano, kifungu cha kuachiliwa kwa Olmo kilipangwa kumalizika Julai 15, lakini kwa sababu bado yuko na Hispania kwenye Euro 2024 kabla ya fainali Jumapili, na sasa imepangwa hadi Julai 20.

Olmo anajiandaa kukabiliana na Kyle Walker wa City, John Stones, na Phil Foden katika fainali itakayofanyika Berlin wikendi hii.

Yeye na Lamine Yamal wa Barca wote walifunga wakati La Roja ikishinda 2-1 dhidi ya Ufaransa.

Licha ya kuanza kwenye benchi kwa mechi tatu kati ya nne za kwanza za Hispania, Olmo amechangia jumla ya mabao matatu na asisti mbili kwenye michuano hiyo.

## Rais Athletic akerwa sakata la Williams

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Athletic Club, Jon Uriarte amekosoa vikali shirikisho la soka la Hiaspania (RFEF) kwa kushindwa kumkinga Nico Williams kutokana na maswali mengi kuhusu mustakabali wake.

Williams amekuwa nyota bora wa Hispania msimu huu wa joto, akijitolea vyema katika safu ya ushambuliaji.

Michango yake imeisaidia Hispania kutinga fainali ya Euro 2024, ambapo wanatarajiwa kucheza na England kesho Jumapili.

Na kutokana na uchezaji wake wa kuvutia, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amekabiliwa na maswali kadhaa kutoka kwa vyombo vya habari kuhusu kama atasalia Athletic, au uwezekano wa kujiunga na mchezaji mwenzake wa Hispania, Lamine Yamal katika klabu ya Barcelona.

Katika taarifa yake, Uriarte alisema (kupitia ESPN): "Nico ni mchezaji anayejitolea kwa Athletic. Amekuwa akikabiliwa na maswali mengi kuhusu mustakabali wake kwa njia ya kupita kiasi na isiyodhibitiwa akiwa kwenye michuano ya Ulaya. RFEF hawajamlinda.

"Heshima kati ya wachezaji wote wanaounda soka ni msingi wa kimsingi - au ndivyo tunavyoiona Athletic - ambayo haijumuishi kuwaweka wachezaji wenye mikataba katika klabu moja kwa shinikizo la umma kujiunga na klabu nyingine."

Williams aliahidi mustakabali wake Athletic mwishoni mwa mwaka jana, akiamua kuongeza mkataba wake hadi 2027 badala ya kuuacha uvurugike na uwezekano wa kuondoka kama mchezaji huru.



HABARI MICHEZO

## Simba yatamba

INATOKA UKURASA 24

"Tumefanikiwa kuinasa saini ya mlinzi wa kulia wa Singida Fountain Gate kwa mkataba wa miaka miwili," ilisema taarifa ya Simba.

Kijili mwenye umri wa miaka 24 ni kijana mwenye kipaji na kasi amekuwa akitumika kuanzisha mashambulizi kutokea upande wa kulia na msimu uliopita amesaidia timu yake ya zamani pasi za mwisho, 'asisti' nne.

Wanachama na mashabiki wa Simba kwa misimu mitatu sasa wamekuwa wakilalamika Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala' kutokuwa na mbadala.

Ujio wa mchezaji huyo na Mburkina Faso, Valentin Nouma, beki wa kushoto kutoka FC Saint Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, umeonekana kuwafurahisha.

Simba imeweka kambi ya wiki tatu kwenye jiji la Ismailia nchini Misri kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa.

Kikosi cha Simba kinatarajiwa kurejea nchini siku chache kabla ya kilele cha tamasha la kila mwaka la klabu hiyo 'Simba Day' litakalofanyika Agosti 3 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

## Yanga: Hatutaidharau Vital'o

INATOKA UKURASA 24

Yanga inatarajiwa kuanza mechi yake ugenini, kati ya Agosti 16 hadi 18, huku mechi ya marudiano ikitarajiwa kuchezwa nyumbani kati ya Agosti 23 mpaka 25.

Yanga inaanzia raundi ya awali, ambapo kama itafanikiwa kupita, itakwenda moja kwa moja raundi ya kwanza na kucheza kukutana na mshindi kati ya SC Villa ya Uganda na  Commercial Sports ya Ethiopia.

Msimu uliopita, Yanga iliishia katika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo na kuondoshwa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwa mikwaju ya penalti 3-2, baada ya suluhu mechi zote mbili zilizochezwa nchini na baadaye Sauzi.

Wakati huo huo, klabu hiyo imemtangaza mchezaji Duke Abuya, raia wa Kenya, akitokea klabu ya Singida Black Stars.

Tayari mchezaji huyo ameshajiunga na wachezaji wengine wa Yanga walioanza mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya Ligi ya Mabingwa na michuano mingine inayowakabili.

Abuya, anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji na wakati mwingine winga, kabla ya kujiunga na Singida, aliwahi kuzichezea klabu za Mathare United, Polisi ya Kenya, Kariobangi Sharks zote za nchini Kenya na Nkana Red Devils ya Zambia.

# COASTAL UNION IMEJIPANGA KIMATAIFA – KOCHA OMNA

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Coastal Union, David Omna amesema kuwa amejipanga vizuri kuhakikisha wanaanza vyema kwenye mchezo wao wa awali wa Kombe la Shirikisho Barani Afrika dhidi ya FC Bravos ya Angola kutokana na mazoezi anayoendelea kuwapa wachezaji wake.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam Kocha huyo aliweka wazi kuwa amefanya usajili mzuri ambao anaamini utaleta mapinduzi makubwa katika mchezo huo.

**"Malengo yangu ni kufanya vizuri kwenye mchezo wetu huo ili tusonge mbele na kwa usajili nilioufanya ninaamini tutapata matokeo mazuri,"alisema Omna.**

Kocha huyo alisema msimu huu amesajili wachezaji wenye viwango vya juu na kudai wengi wao wana uzoefu na mashindano ya Kimataifa.

Aliongeza kuwa anaitumia michuano ya Kagame inayoendelea kama maandalizi ya mchezo huo, kwani wachezaji wake wanajifunza vitu vingi kutoka kwa timu zinazoshiriki.

"Michuano hii inanisaidia kuendelea kuangalia mapungufu na uwezo wa kila mchezaji kabla hatujasafiri kwenda nje ya nchi kwa ajili ya kuweka kambi ya muda," alisema Kocha huyo.

Alisema anawaomba Watanzania waendelee kuwaombea ili waweze kufanikisha malengo yao ili waipeperushe vizuri bendera ya Taifa.

Alisema kila kitu kinawezekana na kusema mpinzani wake ana wachezaji wazuri hivyo amewataka wachezaji wake kuwa na tahadhari kubwa.



Kikundi cha ngoma cha Wagika, kikishangilia na kombe lao baada ya kuibuka washindi katika Tamasha la Kimataifa la Utamaduni na Utalii lililofanyika katika Uwanja wa CCM Bariadi mkoani Simiyu, ikiwa ni katika kuenzi utamaduni wa Wasukuma Kanda ya Ziwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Uhamiaji FC hawatafanya makosa CAF*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Uhamiaji FC, Abdulsaleh Abdallah amesema hawataki kufanya makosa katika mchezo wao wa kwanza wa Kombe la Shirikisho Barani Africa..

Uhamiaji FC itakutana na timu kutoka Libya japo bado hawajaijua timu gani.

Uhamiaji itashuka uwanjani kati ya Agosti 17 na 18 mwaka huu katika uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili Kocha huyo alisema kwa mara ya kwanza timu hiyo inashiriki mashindano hayo makubwa hivyo nia yao kubwa ni kuona wanafanya vizuri katika hatua hiyo ya awali.

Alisema kuanzia nyumbani katika mchezo wao wa kwanza utawapa faida kubwa hasa katika kuwasoma wapinzani wao.

Alisema kupitia mchezo huo utawapa mbinu ambazo wataenda nazo ugenini kuhakikisha wanafanikiwa kupata ushindi.

Alisema wanakabiliwa na mchezo mgumu kwa kuwa soka la nchi hiyo limepiga hatua hasa katika mashindano kama hayo.

"Tunakutana na timu ambayo inatoka katika nchi ambayo kila mtu anajua soka la nchi hiyo, licha ya kutoijua timu gani lazima tuwe na maandalizi ya kutosha,"alisema.

Hata hivyo alisema ingawa ni wanageni katika mashindano hayo hiyo haimaanishi kama watashindwa kutimiza lengo la kusonga mbele.

# Michezo

Jumamosi Julai 13 2024

Nipashe




Van de Beek ni mali ya Girona UKURASA 22



Wachezaji wa Simba wakiendelea na mazoezi yao ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa katika jiji la Ismailia nchini Misri. **PICHA: SIMBA**

## Yanga: Hatutaidharau Vital'0

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya droo iliyofanyika jijini Cairo nchini Misri juzi, ambapo Mabingwa wa Tanzania Bara, imepangwa kucheza dhidi ya Vital'0 ya Burundi, klabu ya Yanga imesema itakwenda kucheza na timu hiyo kwa tahadhari na wala hawatoidharau.

Klabu hiyo imesema ingawa baadhi ya wachambuzi wanaona kama timu hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni mchekea, lakini watakuwa makini kuelekea kwenye mchezo huo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa timu hiyo, Ali Kamwe, amesema kwa sasa akili yao yote inaziwaza dakika 180 za mechi hiyo, ambazo kama wanapita ndizo zitawapa mwangaza kwa nini cha kufanya kwenye mchezo unaofuata.

"Droo tumeipokea vizuri, bahati nzuri imepangwa tukiwa tumeshaanza mazoezi yetu ya kwanza, hivyo tulikuwa tunaishuhudia kwa pamoja hapa Kigamboni pamoja na wachezaji, benchi la ufundi na viongozi.

Kitu ambacho tumekubaliana na kusahau msimu mzuri ambao tumeupitia kwenye Ligi ya Mabingwa msimu uliopita ya kufika mpaka robo fainali, tumekubaliana kuanza upya, kuanza kuhesabu hatua zingine kwa sababu tuna ndoto za kufanya makubwa msimu unaokuja kwenye michuano hiyo, ikiwa ni pamoja na kupita hatua tuliyoiweka msimu uliopita," alisema Kamwe.

Alisema kutokana na hilo, wako makini sana na mchezo ambao watacheza dhidi ya Vital'0, ambao ndiyo utawapa mwanga wa nini watakwenda kukifanya msimu ujao

"Akili yetu sasa inaziwaza dakika 180 hizi dhidi ya Vital'O, tukishamaliza ndipo tutaanza kuangalia mchezo unaofuata utakuwaje," alisema.

ENDELEA UKURASA 23

# SIMBA SC YAJIGAMBA KUONESHA UKUBWA CAF

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

### ●●● Yachekelea droo, yatangaza kumsajili msaidizi wa Kapombe huku...

SIKU moja baada ya droo ya michuano kombe la Shirikisho Afrika kupangwa, uongozi wa klabu ya Simba umesema umepokea kwa furaha ratiba ya michuano hiyo kwa kuwa wanaenda kukutana ma timu ambazo zipo chini yao kiuwezo kwenye hatua ya kwanza.

Katika droo iliyochezeshwa makao makuu ya CAF, Cairo, Misri, Simba ambayo itaanzia hatua ya kwanza, inasubiri kucheza na mshindi kati ya Uhamiaji FC ya Zanzibar na muwakilishi kutoka Libya ambaye bado hajajulikana kwenye mchezo wao wa hatua ya awali.

Meneja wa habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally aliiambia Nipashe kuwa njia kwao ni nyeupe kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

**"Tumepokea vizuri droo ya CAF, hatuwadharau wapinzani, yoyote atakayekuja tunadili naye, kwetu tunaona njia nyeupe kwenda hatua nyingine, tunasubiri mpinzani wetu aje na tutampokea," alisema Ahmed.**

Alisema kwa timu yoyote itakayofuzu kwenda kucheza nao, hawatamdharau kwa kuwa ni timu ndogo kwao kwa sababu mchezo wa mpira ni mchezo wa makosa.

"Hizi timu ndogo hatupaswi kuzidharau, ukizidharau wanaweza kukuvua nguo ukweni, kwa hiyo tunajiandaa vizuri, kama mnavyojua tayari timu imeanza maandalizi ya Ligi Kuu pamoja na michuano hii," alisema Ahmed.

Alisema kwa sasa kazi inaendelea kukiandaa kikosi chao kuelekea kwenye msimu mpya wa mashindano.

"Mazoezi yanaanza kupamba moto kwenye kambi yetu, kila mchezaji ana morali ya hali ya juu, na kocha wetu mpya Fadlu Davids amefurahishwa na hali aliyoikuta kwa wachezaji wake," alisema Ahmed.

"Kusema kweli kocha ameshaanza mazoezi na ameonesha kufurahishwa na viwango vya wachezaji aliowakuta na kusema ana kazi ya kukiunganisha ili kucheza katika mfumo anaouhitaji."

Wakati huo huo, klabu hiyo imetangaza kumsajili beki wa kulia Kelvin Kijili, kutoka klabu ya Singida Fountain Gate.

Kijili amejiunga na klabu hiyo kwa mkataba wa miaka miwili na kazi yake kubwa itakuwa kwenda kuungana na Shomari Kapombe upande wa kulia wa kikosi hicho.

ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >